# HADITHI ZA KUMHUSU DAJALI KATIKA SUNNAH YA NABII

## NA KUZIBAINISHA KWA RAMANI ZA KILEO





UTUNZI WA

DKT. ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD AL-QAASIM

IMAMU NA HATIBU WA AL-MASJID AN-NABAWI SH-SHARIIF

# HADITHI ZA KUMHUSU DAJALI KATIKA SUNNAH YA NABII NA KUZIBAINISHA KWA RAMANI ZA KILEO

Inawezekana kuangalia na kuteremsha vitabu vyote vya fadwilatu Shaikh katika kiunganishi:

a-alqasim.com/books/

# HADITHI ZA KUMHUSU DAJALI KATIKA SUNNAH YA NABII NA KUZIBAINISHA KWA RAMANI ZA KILEO

**Utunzi**

**Sheikh Dakturi/ Abdul-Muhsin Muhammad Al-Qasim**

**Imamu na hatibu wa msikiti wa Nabii mtukufu**

بسم الله الرحمن الرحيم

NAANZA KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

## UTANGULIZI

Sifa njema zote ni za Allah Mola mlezi wa viumbe wote, na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, jamaa zake na masahaba wake wote.

Ama baada ya himdi hii:

Basi hakika jambo la Kiyama ni adhimu, na kwa rehema yake aliyetakasika alikijaalia Kiyama kuwa na alama; ili waja warudi kwazo, na wajiandae kwa ajili ya hesabu [ya siku hiyo], na kama alivyojaalia Kiyama kuwa na alama; vilevile amezijaalia alama zake [hizo] kuwa na alama kwazo zinatambulika, na ni miongoni mwa alama za Kiyama ambazo zinao alama ni: Kutoka kwa masihi dajali.

Na kwa ajili ya fitina yake kubwa kila Nabii alitahadharisha umma wake naye, na Nabii [Muhammed] swala na salamu za Allah zimshukie alitutahadharisha naye na akabainisha shani yake kwa alama zilizowazi kabisa.

Na ni kwa ajili ya uhatari wa fitina yake ndio nimekusanya Hadithi sahihi zilizokuja kumhusu masihi dajali, na nikabainisha misamiati yake, na zile ambazo mnao ndani yake kutaja sehemu nimebainisha sehemu hizo kwa ramani na picha, na nikataja sababu za kusalimika kutokana naye; ili yakini ya Mwislamu izidi kuwa yeye ni dajali; ndiposa apate kuwa na hadhari naye, na aepuke fitina yake, na nikakiita: ((HADITHI ZA [KUMHUSU] DAJALI KATIKA SUNNAH YA NABII NA KUZIBAINISHA KWA RAMANI ZA KILEO))

Namuomba Allah anufaishe kupitia kitabu hiki, na atulinde kutokana na fitina ya Masihi dajali.

Na swala na salamu za Allah zimshukie Nabii wetu Muhammad, jamaa zake na masahaba wake wote.

Dr. Abdul-Muhsin ibnu Muhammad Al-Qasim

Imamu na hatibu wa Msikiti mtukufu wa Nabii

Nilikimaliza tarehe ishirini na tano ya mwezi wa Rajabu,

mwaka elfu moja mia nne na arobaini na tatu hijria.

## HATUA ZA KITABU

Nimekigawanya kitabu hiki katika sura kama ifuatavyo:

**Sura ya Kwanza**: Jina la Masihi dajali.

**Sura ya pili**: Sababu ya kuitwa (Masihi dajali).

**Sura ya tatu**: Kuthibiti hadith zinazomhusu Masihi dajali.

**Sura ya nne**: Masihi dajali ni miongoni mwa alama kubwa za Kiyama.

**Sura ya tano**: Tahadhari kutokana na Masihi dajali.

**Sura ya sita**: Hofu ya masahaba kutokana na fitina ya Masihi dajali.

**Sura ya saba**: Sifa za Masihi dajali.

**Sura ya nane**: Uhakika wa Masihi dajali.

**Sura ya tisa**: Udhaifu wa Masihi dajali.

**Sura ya kumi**: Hali ya Masihi dajali sasa hivi.

**Sura ya kumi na moja**: Alama za kutoka masihi dajali.

**Sura ya kumi na mbili**: Lini Masihi dajali atatoka.

**Sura ya kumi na tatu**: Sababu ya kutoka Masihi dajali.

**Sura ya kumi na nne**: Sehemu ya kutokea Masihi dajali.

**Sura ya kumi na tano**: Hali ya watu pindi atakapotoka Masihi dajali.

**Sura ya kumi na sita**: Kasi ya kutembea Masihi dajali katika ardhi.

**Sura ya kumi na saba**: Masihi dajali hatoingia Makkah wala Madinah.

**Sura ya kumi na nane**: Madinah haitoingiwa na hofu ya Masihi dajali.

**Sura ya kumi na tisa**: Sehemu ya kando ya Madinah atakayoshukia Masihi dajali.

**Sura ya ishirini**: Muda atakaookaa Masihi dajali katika ardhi.

**Sura ya ishirini na moja**: Fitina ya Masihi dajali.

**Sura ya ishirini na mbili**: Hekima katika fitina ya Masihi dajali.

**Sura ya ishirini na tatu**: Hukumu ya kumfuata Masihi dajali.

**Sura ya ishirini na nne**: Mtu atakayekuwa mkali zaidi juu ya dajali.

**Sura ya ishirini na tano**: Sababu ya kuokoka kutokana na fitina ya Masihi dajali.

**Sura ya ishirini na sita**: Mauwaji ya Masihi dajali.

**Sura ya ishirini na saba**: Ramani za kubainisha sehemu zilizotajwa katika hadithi zinazomhusu Masihi dajali.

❊❊❊

## JINA LA MASIHI DAJALI

Masihi dajali ameitwa kwa sifa zilizotangaa zaidi; na anao majina manne:

1. MASIHI DAJALI.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Takeni ulinzi kwa Allah kutokana na fitina ya Masihi dajali**)), imepokewa na Muslim[1].

2. MASIHI WA UPOTEVU.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Masihi wa upotevi atatoka upande wa mashariki**)), imepokewa na ibnu Hibbaan.[2]

3. CHONGO DAJALI.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika chongo dajali - masihi wa upotevu - atatoka upande wa mashariki, katika wakati wa hitilafu na mfarakano wa watu**)), imepokewa na ibnu Hibbaan[3].

4. CHONGO MUONGO.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hajawahi kutumilizwa Nabii yeyote ila alionya umma wake kutokana na chongo muongo**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[4].

---

1 Muslim, nambari (588), katika hadithi za Abu Huraira Allah amridhie.

2 Ibnu Hibbaan, nambari (6812), katika hadithi ya Abu Huraira Allah amridhie

3 Marejeo yaliotangulia.

4 Bukhari, nambari (7131), na Muslim, nambari (2933), katika hadithi za Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

Na haikusihi kumwita (Masikhi Dajali).

Ibnu Abdil-Bar Allah amrehemu amesema: "Na walikuwa baadhi ya wapokezi wa hadithi wakimwita Dajali: Al-Misiha.

Na kati yao mna waliosema hilo kwa 'kha' [yaani: Al-Misikha].

Na hayo yote ni makosa mbele ya wenye ilimu"[1].

❉❉❉

1 At-Tamhiid (14/188).

## SABABU YA KUITWA «MASIHI DAJALI»

Jina la Masihi dajali limepandanishwa kutokana na maneno mawili:

mojawapo ni «Masihi», na lengine ni «Dajali», na kila moja lina maana na sababu ya kuitwa nalo.

**Kwanza**: sababu ya kuitwa «Masihi»

1- Kwa ajili ya kukata masafa ya ardhi kwa muda mfupi: yaani ataizunguka [ardhi] na ataingia miji yote isipokuwa Makkah na Madinah.

2- Na imesemekana : Ni kwa ajili ya kuwa yeye amefutwa jicho moja [chongo wa jicho moja][1].

**Pili**: Sababu ya kuitwa ((Dajali)):

1. Kwa sababu yeye ni muongo, kwani Dajali hudanganya watu.

2. Na imesemwa: Kwa sababu ya kuwakanganya watu na kuwatatiza[2].

Na amesifiwa kwa [sifa ya] Dajali; ili atofautike na Masihi mwana wa Maryam salamu zimshukie.

❉❉❉

1 At-Tamhiid (14\188), Tafsiirul Qurtuby (4/89).

2 Sharhu Ssunnah (15/27), Kashful mushkili min hadiithi Sswahiiheini (1/382), na Fat-hul baari, ya ibnu Hajar (13/91).

# KUTHIBITI HADITHI ZA MASIHI DAJALI

Hadithi zilizokuja kuhusu Masihi dajali ni hadithi sahihi mutawatirah - zilikuja kwa njia nyingi, ni muhali waafikiane wapokezi wake juu ya urongo-, na mwenye kuzikanusha hana hoja, ibnu Kathiir (amekufa 774 hijria) Allah amrehemu amesema: "Ama hadithi zinazomtaja dajali peke yake ni nyingi sana, nazo ni nyingi mno kiwango cha kutoweza kuhesabika, kwa ajili ya kuenea kwake na wingi wa wapokezi wake katika vitabu vya sahihi, hasan, masaaniidi na vyenginevyo"[(1)].

Na akasema tena Allah amrehemu: "Na kuna mapote mengine miongoni mwa khawaarij, jahmiyyah na baadhi ya mu'tazila wamepinga kabisa kutoka kwa Dajali, na wakazikataa hadithi zilizokuja kumhusu, basi hawakufanya kitu, na kwa hilo wametoka katika boma la wanazuoni; kwa kule kukataa kwao jambo ambalo zimekithiri kulihusu habari sahihi tena kwa njia isiokuwa moja kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie "[2]

Na Al-Kattaani (amekufa 1345 hijria) Allah amrehemu amesema: "Hadithi za kutoka kwa Masihi dajali: Wametaja [ulamaa] zaidi ya mmoja ya kwamba zimekuja kwa njia nyingi zilizo sahihi kupokewa masahaba wengi, na katika kitabu 'At-Tawdwiih'[(3)] cha Shawkaani zipo hadithi mia [za Dajali], nazo zipo katika vitabu vya sahihi, maajimi na masaaniidi, na sifa ya

---

1 Tafsiir ibnu Kathiir (2/464).

2 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/193).

3Yaani kitabu cha: At-Tawdwiih fii tawaaturi maa ja-a fil mahdiyyil muntadwar wa ddajjaal, wal Masiih', nacho ni kitabu ambao bado kipo katika hali ya hati za mkono, ipo nuskha yake katika maktaba ya sheikh Hammaad Al-Answaari Allah amrehemu.

Tawaaturu hupatikana kwa idadi duni yake, basi iweje zinapokusanyika zote?!

Na Baadhi yao [wanazuoni] walisema: Habari za Dajali zinahimili kuwa katika mijeledi mingi, na zaidi ya mmoja katika maimamu wamezitengea utunzi"[1] .

Basi ikisemwa: Kwanini Dajali hakutajwa wazi katika Qur-ani tukufu?

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Hakutajwa wazi katika Qur-ani kwa jina lake ili kumdunisha,kwa kuwa yeye anadai haki ya kuabudiwa [Uola] naye ni mtu, naye pamoja na utu wake ni mpumgufu wa umbile, basi hali yake mbele ya Mola Mlezi ni duni zaidi ya [kustahiki] kutajwa, na ni ndogo zaidi na dhalili zaidi ya madai yake [kustahiki] kunyanyuliwa na kutahadharishwa.

Lakini Mitume walitetea heshima ya Mola Mlezi mwenye izza na utukufu, basi wakawaekea wazi kaumu zao hali yake [dajali], na wakawatahadharisha fitina potovu alizonazo.

Basi ikatosha kutoa habari kwa Manabii, na kuja habari kwa wingi kutoka kwa bwana wa wanadamu na imamu wa wachamgu; kuliko itajwe amri yake duni ukilinganisha na utukufu wa Allah katika Qur-ani tukufu, na kazi ya kubainisha amri yake ikategemezwa kwa kila Nabii mkarimu.

Na ukisema: Hakika ametajwa firauni ndani ya Qur-ani, na amedai aliyoyadai katika haki ya kuabudiwa na urongo na uzushi aliposema:

﴿فَقَالَ أَنَا۠ رَبُّكُمُ ٱلۡأَعۡلَىٰ﴾

{Hakika mimi ni mola wenu aliyejuu kabisa} [An-Naazi'at: 24].

1 Nadhmul mutanaathir (uk 228).

Basi jibu ni: Kuwa amri ya firauni imeisha, na umebainika uongo wake kwa kila muumini na mwenye akili, na amri ya dajali itakuja [haijaisha]"[1].

❉❉❉

1 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/197).

## MASIHI DAJALI NI KATIKA ALAMA KUBWA ZA KIYAMA

Kinao Kiyama alama ndogo na kubwa, na pindi alama kubwa za Kiyama zitadhihiri basi Kiyama kitasimama, na ni miongoni mwa alama kubwa za Kiyama: Kutoka kwa Masihi dajali, na katika dalili zilizokuja katika hilo ni:

1. Hudheifa ibnu Asiidi Al-Gifaari Allah amridhie alisema: ((Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alitutokea nasi tukiwa tunakumbushana, akasema: **Mnakumbushana nini?** Wakasema: Tunakumbushana Kiyama.

Akasema: **Hakika hakitasimama hadi muone kabla yake alama kumi.**

**Akataja: Moshi, Dajali, mnyama [atakayezungumzisha watu], kuchomoza jua kutoka magharibi yake, kushuka kwa Isa ibnu Maryam swala na salamu za Allah zimshukie, Yajuuja wa Majuuja, mididimio mitatu: mdidimio utakaokuwa mashariki, mdidimio utakaokuwa magharibi na mdidimio utakaokuwa uarabuni, na ya mwisho ni: Moto utakaotoka Yemen utakaofukuza watu kuwapeleka sehemu yao ya kukusanywa**)), imepokewa na Muslim[1].

2. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Mambo matatu yanapotoka**

﴿لَا يَنفَعُ نَفْسًا إِيمَٰنُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِن قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِيٓ إِيمَٰنِهَا خَيْرًاۗ﴾

**{kuamini hapo hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake}[Al-An'am: 158], kuchomoza jua kutoka magharibi,**

1 Muslim, nambari (2901).

**Dajali, na mnyama wa ardhini**)), imepokewa na Muslim[1].

1 Muslim, nambari (158), katika hadithi za Abu Huraira Allah amridhie.

## KUTAHADHARISHA KUTOKANA NA MASIHI DAJALI

Manabii walionya umma zao kutokana na Masihi dajali kwa ajili ya nguvu ya fitina yake, na ulamaa wametembea juu mwendo huu katika kutahadharisha watu naye, na ubainifu wa hilo ni katika yafuatayo:

1. Manabii salamu ziwashukie walikuwa wakitahadharisha kaumu zao kutokana na dajali, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakuna Nabii ila ameutahadharisha umma wake kutokana na chongo muongo, basi jueni kuwa yeye ni chongo, na hakika Mola wenu Mlezi si chongo, [Dajali] ameandikwa baina ya macho yake [kaa faa raa]**)) wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na Muslim akaongoza: ((**Jifunzeni**[1] **kuwa katu mmoja wenu hatamuona Mola wake hadi afariki**))[2].

Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema (amefariki 852 hijria): "Kauli yake: (yeye ni chongo, na hakika Allah si chongo), amekomea katika hilo pamoja na kuwa dalili za kuumbwa katika dajali zipo wazi; kwa kuwa uchongo ni athari ya kihisi, inajulikana na mwenye elimu, asiye na elimu na asiye weza kutambua dalili za kiakili. Basi akidai Uola na hali yeye ni mpungufu wa umbile, na Mola mwabudiwa ametakasika kutokana na upungufu; itajulikana wazi kuwa yeye ni mrongo.

Na mnao ndani yake: Tanabahisho la kuwa kudai kwake Uola ni urongo; sababu kumuona Allah aliyetukuka

---

1 Jifunzeni: Jueni.

2 Bukhari, nambari (3057), na Muslim, nambari (2931}, katika hadithi za ibnu Umar Allah awaridhie.

kumefungamanishwa na kufa, na dajali atadai kuwa yeye ni Allah, na pamoja na hivyo watu watamuona"[1].

2- Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ameutahadharisha umma wake naye, akasema: ((**Hakika mimi nawaonya naye, hakuna Nabii ila ameonya kaumu yake naye, Hakika Nuuh ameionya kaumu yake naye.**

**Lakini nitawaambia kumhusu kauli ambayo hajawahi Nabii yeyote kuiambia kaumu yake, jifunzeni[2] kuwa yeye ni chongo, na hakika Allah aliye mwingi wa baraka na aliyetukuka si chongo**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[3].

Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: "Na imesemekana: Kuwa siri ya kuhusishwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na tanabahisho lililotajwa [katika hadithi] pamoja na kuwa hilo ni miongoni mwa dalili za wazi kabisa katika kumkadhibisha Dajali; ni kuwa Dajali atatokeza katika umma wake, wala sio umma nyenginezo zilizotangulia.

Na hadithi ikajulisha: kuwa kujua ya kwamba kutoka kwake ni mahsusi na umma huu, basi hilo lilifichwa kwa umma nyenginezo, kama ilivyofichwa kujua wakati wa kusimama Kiyama kwa wote"[4].

3- Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aeleza ukubwa wa fitina yake, akasema: ((**Hamna baina ya kuumbwa Adam hadi kusimama kwa Kiyama kiumbe kikubwa kuliko Dajali**)),

1 Fat-hul baari (13/96).

2 Jifunzeni: jueni.

3 Bukhari, nambari (3057), na Muslim, nambari (2931), katika hadithi za ibnu Umar Allah awaridhie.

4 Fat-hul baari (13/96).

imepokewa na Muslim, na katika riwaya yake nyengine: ((**Jambo kubwa kuliko Dajali**))[1].

Yaani: Hamna baina ya kuumbwa Adam hadi kusimama kwa Kiyama fitina kubwa zaidi kuliko Dajali; kwa ajili ya ukubwa wa fitina yake na balaa yake, na kwa ajili ya wingi wa utata wake na mitihani yake[2].

Al-Qaadhi ‘Iyaadh Allah amrehemu (amekufa 544 hijria) amesema: "Kauli yake: ((kubwa kuliko Dajali)), huo ni ukubwa wa jambo lake na fitina yake, wala si ukubwa wa kimwili; hili ndilo linalodhihiri.

Na inamkini: kuwa anaashiria ukubwa wa mwili"[3].

4- Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anajilinda na Allah kutoka naye [Dajali] katika Swala, Aisha Allah amridhie amesema: ((Nimemsikia Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akijilinda na Allah katika swala yake kutokana na fitina ya Dajali)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[4].

5- Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ameamrisha umma wajilinde na Allah kutokana naye [Dajali], akasema: ((**Jilindeni na Allah kutokana na adhabu ya Allah, jilindeni na Allah kutokana na adhabu ya kaburi, Jilindeni na Allah kutokana na fitina ya Masihi dajali, Jilindeni na Allah kutokana na fitina ya uhai na mauti**)), imepokewa na Muslim[5].

---

1 Muslim, nambari (2946), miongoni mwa hadithi za Imran ibnu Huswein Allah awaridhie.

2 Mirqaatul mafaatiih: (8/3452).

3 Ikmaalul mu'lim bifawaaidi muslim: (8/504).

4 Bukhari, nambari (832), na Muslim, nambari (587).

5 Muslim, nambari (588), miongoni mwa hadithi za Abu Huraira Allah amridhie.

6- walikuwa wanazuoni wakiamrisha kuwakumbusha watu Masihi dajali punde baada ya punde; ili watahadhari fitina yake, As-Safaariini Allah amrehemu (amekufa: 1188 hijria) amesema: "Ni katika yanayompasa kila mwanachuoni aeneze hadith za kumhusu Dajali baina ya watoto, wanawake na wanaume, hasa hasa katika wakati wetu huu ambao fitina zimenyanyuka ndani yake, na mitihani imekithiri, na alama za sunnah zimefutika[1].

❉❉❉

1 Lawaamiul anwaaril bahiyyah (2/106).

## HOFU YA MASAHABA ALLAH AWARIDHIE KUTOKANA NA FITINA YA MASIHI DAJALI

Masahaba allah awaridhie walikuwa wakikumbushana Masihi dajali kwa kuogopea fitina yake, na yamejulisha hilo yanayofata:

1. Abu Said Al-Khudry Allah amridhie amesema: ((Tulikuwa tukishika zamu ya kulala kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie; akiwa na haja, au akifikwa na jambo usiku akitutuma, basi wakakithiri wenye kutaka ujira wa hilo na wenye kushika zamu[1].

Basi tukawa tunazungumza, Mtume akatutokea usiku, akasema: **Ni mnongono gani huu?**

Asema: Tukasema: Tunatubia kwa Allah ewe Nabii wa Allah, hakika tulikuwa katika (mazungumzo ya) kumtaja Dajali kwa kumuogopa.

Basi akasema: **Siwapeni habari ya jambo ambalo linahofisha zaidi kuliko Masihi dajali?**

Akasema: Tukasema: kwani [tujuze].

Akasema: **Ni shirki ya kufichana, nayo ni mtu asimame kufanya amali kwa ajili ya mtu**)) imepokewa na Ahmad[2].

2. Amepokewa An-Nawwaas ibnu Sam'aan Allah awaridhie kuwa amesema: (Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alimtaja Dajali asubuhi moja, basi akateremsha ndani yake[3] na akanyanyua [4], hadi tukadhani yupo katika upande wa

1 **Wenye kushika zamu**: Ni wanaume ambao wanashika zamu ya ulinzi kila usiku.
2 katika Musnad, nambari (11252).
3 **Akateremsha**: Akadunisha amri yake.
4 **Akanyanyua**: Akaadhimisha fitina yake.

mitende [yaani: karibu yao].

Tulipomwendea alijua hilo kwetu, basi akasema: **Mna nini?**

Tukasema: Ewe Mtume wa Allah, Ulimtaja Dajali asubuhi, na ukateremsha sauti na kupandisha, hadi tukadhani kuwa yupo katika upande wa mitende!

Basi akasema: **Anayeogopesha kwenu zaidi ni mwengine asiyekuwa Dajali; kwani akitoka nami nipo miongoni mwenu; basi mimi nitamghilibu kihoja nikiwa mbele yenu na nitawakingeni**.

**Na akitoka nami sipo na nyinyi; basi kila mmoja ni mwenye kujitetea nafsi yake, na Allah ndiye halifa wangu juu ya kila Mwislamu** [1])), imepokewa na Muslim[2].

❉❉❉

1 **Halifa wangu juu ya kila Mwislamu**: Allah ndiye mwenye kumnusuru kila Mwislamu na mwenye kumhifadhi.

2 Muslim, nambari (2937).

## SIFA ZA MASIHI DAJALI

Sunnah ya Nabii imekuja kubainisha sifa za Dajali ili Muumini amtahadhari; Abu Abdillah Muhammad Al-Qurtubi (671 hijria) Allah amrehemu amesema: "Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ameelezea wasifu wa Dajali kiasi cha kuwa hakuacha utata wowote kwa mwenye akili, na sifa hizo zote ni mbovu, zinabainika kwa kila mwenye hisia iliyosalimika, lakini yule ambaye Allah ashamuhukumia uovu basi atamfuata Dajali katika anayoyadai miongoni mwa uongo na upumbavu, na atanyimwa kufuata haki na nuru ya kufuata [sunnah] (1)", na sifa hizo ni:

1. **Mwili mkubwa**:

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema akitoa habari kuhusu aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie: ((**Basi tukatembea kwa haraka, hadi tukaingia kasri kubwa, mara ndani yupo mtu mkubwa wa umbile hatujaona mfano wake katu**)), imepokewa na Muslim.

2. Mtu mwenye Rangi Nyekundu; yaani: Weupe unaomailika katika wekundu .

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: **((Kisha nikageuka; mara tu naona mtu mwekundu mwenye mwili mkubwa**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

3. Chongo; Kana kwamba jicho lake ni zabibu iliyochomoza.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie

1 At-Tadhkiratu fii ahwaalil mawtaa wa umuuril aakhirah, (uk: 1279).

amesema: ((**Na Masihi dajali ni A'war [chongo] wa jicho la kulia, kana kwamba jicho lake ni zabibu iliyochomoza** [(1)])), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na katika mapokezi ya Muslim: ((**Dajali ni A'war [mbovu] wa jicho la kushoto**)).

Ibnu Abdi-Ddaaim (amekufa: 831 hijria) Allah amrehemu amesema: "A'war katika kila kitu ni: kibovu chenye kasoro, na macho ya Dajali yote mawili ni yenye kasoro: mojawapo ni kwa kutoona kwake, na lengine ni kwa kule kuchomoza kwake na ubovu wake"[(2)].

Na Al-Mudh-hiry (amekufa: 727 hijria) Allah amrehemu amesema: "Basi kukisemwa: Ni nini hekima ya kuwa ameumbwa akiwa chongo mwenye ubovu wa jicho? Basi itajibiwa: Hata lau yeye angesibiwa na maafa mengine kando na ubovu wa jicho, basi hayangedhihiri kama vile unavyodhihiri ubovu wa jicho, au ni kuwa huo [ubovu wa jicho] unakuwa ni alama inayojulisha uongo wake na uchawi wake.

Na lau itasemwa: Lau angekuwa kipofu basi angedhihiri zaidi kuliko kuwa mbovu wa jicho?

Basi itajibiwa: Ni kwa sababu ya kuwa Allah aliyetakasika amekadiria kuwapoteza kwaye kaumu ya watu, na lau angekuwa kipofu basi haingepatikana kutoka kwake kupoteza na kupotosha"[(3)].

4. Juu ya jicho lake chongo mna gozi gumu linalofunika jicho.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie

---

1 Na katika riwaya: iliyopoteza nuru.

2 Al-Laamiu sswabih bisharhil jaamiu sswahih, (10/27).

3 Al-Mafaatiih fii sharhil masaabiih, (5/409).

amesema: ((**Hakika Dajali amefutwa jicho** [1]**, juu yake mna gozi gumu**)), imepokewa na Muslim.

5. Baina ya macho yake amendikwa: (kaaf faa raa), yaani: kafiri, kila Mwislamu atalisoma [andiko hilo].

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Dajali amefutwa jicho, ameandikwa baina ya macho yake 'kafiri', kisha akataja herufi zake (kaaf faa raa), kila Mwislamu atalisoma**)), imepokewa na Muslim.

6. Ni mwingi wa nywele.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Dajali ni mbovu wa jicho la kushoto, mwingi wa nywele**)), imepokewa na Muslim.

7. Nywele za kichwa chake ni ngumu sana, si za kutiririka, na Masihi dajali ni mtu mwekundu, na nywele ngumu hazinasibiani na mtu mwekundu; basi hii ni sifa ya ubovu[2].

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Na nikamuona nyuma yake mtu mwenye nywele ngumu sana**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Al-Qaadhwi 'iyaadh Allah amrehemu amesema: "Mfano wa watu weusi"[3].

8. Hatazaliwa mtoto.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika yeye hatazaliwa mtoto** [yaani: hatapata mtoto])), imepokewa Muslim.

---

1 Amefutwa jicho: Sehemu ya jicho moja imefutwa, mfano wa paji lake [yaani: hakuna hata alama ya jicho].

2 Al-Laamiu sswabih bisharhil jaamiu sswahih, (10/28).

3 Mashaariqul anwaar (2/183).

❋ **Bayana ya hadithi zilizokuja kuhusu hayo ni kama ifuatavyo:**

1- Fatima binti Qais Allah amridhie amesema: ((Nilisikia mwito mwa mpiga mbia - mpiga mbia wa Mtume wa Allah swala na salama za Allah zimshukie - akiita: As-Swalaatu jaamiah, basi nikatoka kuelekea msikitini, nikaswali pamoja na Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, nikawa katika safu ya wanawake ambayo inafuatia migongo ya wanaume [safu ya mbele ya wanawake].

Pindi Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alipomaliza swala yake alikaa juu ya mimbari huku akicheka, na akasema: **Kila mmoja akaye aliposwali**, kisha akasema: **Je mnajua kwa nini nimewakusanya?**

Wakasema: Allah na Mtume wake wanajua Zaidi.

Akasema: **Hakika mimi Wallaahi sijawakusanya kwa kuwatamanisha wala kuwaogopesha, lakini nimewakusanya kwa sababu Tamiim Ad-Daary alikuwa ni mnasara, akaja akatoa bey'a na akasilimu, na akanihadithia hadithi iliyoafiki yale ambayo niliokuwa nikiwahadithia kuhusu Masihi dajali.**

**Amenihadithia kuwa alipanda jahazi pamoja na watu thelathini kutoka kabila la Lakhmi na Judhaam** [1]**, basi mawimbi yakawarusharusha katika bahari mwezi mzima, kisha wakakurubia kisiwa katika bahari hadi jua likachwa.**

**Basi wakaingia katika vijidau vya jahazi lao, wakaingia katika kisiwa, wakakutana na mnyama mwenye nywele ngumu nyingi, hawamtambui mbele yake wala nyuma yake kutokana na wingi wa nywele, basi wakasema: Ole wako wewe ni nini?**

1 **Lakhmi na Judhaam**: Kabila mbili kutoka Yemen.

**Akasema: Mimi ni [Al-Jassaasa] jasusi**[1].

**Wakasema: Al-Jassaasa ni nini?**

**Akasema: Enyi watu nendeni kwa huyu mtu katika kasri, kwani yeye ana shauku mno ya habari zenu.**

**[Tamiim] akasema: alipotutajia mtu tukaogopa asije akawa ni shetani.**

Asema: **Tukaondoka mbio hadi tukaingia katika kasri, mara tu tukaona ndani yake kuna mtu mwenye umbile kubwa sana hatujawahi kuona, amefungwa vigumu sana kwa chuma, mikono yake imekusanywa katika shingo yake, na kufungwa kwa chuma baina ya magoti yake hadi katika visigino vyake**)), imepokewa na Muslim[2].

2. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Nimejiona usiku wa leo ndani ya ndoto nikiwa katika Kaaba** - na katika riwaya yao[3] nyengine: **Nilipokuwa nimelala niliona kuwa naitufu Kaaba** -.

**Mtu mmoja aliyekuwa rangi ya kahawia iliyo mzuri mno, nywele zake zinagusa baina ya mabega yake, nywele zake zimechanwa,** - na katika riwaya nyingine: **mwenye nywele zilizonyooka - kichwa chake kinatona maji, ameweka mikono yake katika mabega ya watu wawili, naye ako baina yake akitufu Kaaba, basi nikasema: Ni nani huyu?**

**Wakasema: ni Masihi Isa ibnu Maryam.**

**Na nikaona nyuma yake mtu aliyekuwa na nywele ngumu sana, mbovu wa jicho la kulia.**

---

1 **[Al-Jassaasa] jasusi**: Ameitwa hivyo kwa sababu anajasusi habari kumpelekea Dajali.

2 Muslim, nambari (2942).

3 Yaani: Bukhari na Muslim.

- na katika riwaya nyengine - **Kisha nikageuka, mara nikaona mtu mwekundu mnene - katika watu niliowaona anafanana zaidi na ibnu Qatwin[1], akiwa ameweka mikono yake juu ya mabega ya watu wawili akitufu Kaaba.**

**Nikasema: Ni nani huyu?**

**Wakasema: ni Masihi dajali**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[2].

3. Ibnu Umar Allah awaridhie amesema: ((Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alisimama kati ya watu akamsifu Allah na sifa anazostahili, kisha akamtaja Dajali - Bukhari amezidisha katika riwaya: akarefusha katika kumtaja -.

Na akasema: **Mimi nakutahadharisheni naye, hakuna Nabii yeyote ila ametahadharisha kaumu yake naye, hakika Nuhu ametahadharisha kaumu yake naye.**

**Lakini nawaambia kumhusu kauli ambayo hajawahi Nabii yeyote kuwaambia kaumu yake: Jueni kuwa yeye ni mbovu wa jito, na kuwa Allah mwingi wa baraka na aliyetukuka si mbovu wa jicho**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[3].

4- Ibnu Umar Allah awaridhie amesema: ((Alitajwa Dajali mbele ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, basi akasema: **Hakika Allah hafichiki kwenu, hakika Allah si mbovu wa jicho** - na akaashiria kwa mkono wake katika jicho lake -.

1 **Ibnu Qatwin** ni: Abdul-uzzaa ibnu Amr wa zama za Jahiliya wa kabila la Khuza'a, mamake ni Haala binti Khuweylid, ndugu ya Khadija binti Khuweylid Allah amridhie.

2 Bukhari, nambari (3440), na Muslim, nambari (169), miongoni mwa hadithi za Umar Allah amridhie.

3 Bukhari, nambari (4402), na Muslim, nambari (169).

**Na Masihi dajali ni mbovu wa jicho la kulia, kana kwamba jicho lake ni zabibu iliyochomoza**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

5- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Dajali ameandikwa baina ya macho yake: (kaaf faa raa), yaani kafiri**)), imepokewa na Muslim[2].

6- Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Ameandikwa baina ya macho yake: kafiri**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[3].

7. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika Dajali amefutwa jicho, juu yake mna gozi gumu, ameandikwa baina ya macho yake: kafiri, kila Muumini atalisoma - anayejua kuandika na asiyejua-**)), imepokewa na Muslim[4].

8- Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Dajali ni mbovu wa jicho la kushoto, mwenye nywele ngumu**)), imepokewa na Muslim[5].

9. Ibnu Saiid Al-Khudry Allah amridhie amesema: "Nilisuhubiana na ibnu Swaaid[6] [katika safari ya] kuenda Makkah, basi akaniambia: Nilikutana na watu wanaodai kuwa mimi ni Dajali, kwani wewe haukumsikia Mtume wa Allah swala

---

1 Bukhari, nambari (7407), na Muslim, nambari (169).

2 Muslim, nambari (2933), miongoni mwa hadithi Anas ibnu Maalik Allah amridhie..

3 Bukhari, nambari (7408), na Muslim, nambari (169).

4 Muslim, nambari (2934), miongoni mwa hadithi za Hudheifa ibnul Yamaan Allah awaridhie.

5 Muslim, nambari (2934), miongoni mwa hadithi za Hudheifa ibnul Yamaan Allah awaridhie.

6 **Ibnu Swaaid**: Jina lake ni Swaaf kutoka kabila la Baany An-Najjaar.

na salamu za Allah zimshukie akisema: Hakika yeye [Dajali] hatazaliwa mtoto?

Nikasema: Kwani [yaani: nimemsikia]

Akasema: Basi mimi nimezaliwa mtoto)), imepokewa na Muslim[1].

❉❉❉

1 Muslim, nambari (2927).

## HAKIKA YA MASIHI DAJALI

Masihi dajali ni katika wanadamu, Allah atawatahini waja wake naye, na atamuezesha juu ya mambo kadhaa, kisha atamnyima.

Al-Qaadhwi 'Iyaadh Allah amrehemu amesema: "Hadithi ambazo Muslim - yaani: imamu Muslim katika kitabu chake cha swahiih - ameziingiza katika kisa cha Dajali ni hoja za watu wa haki katika usahihi wa kuwepo kwake [Dajali], na kuwa ni mtu fulani, Allah amewatahini naye waja wake, na akamuwezesha mambo kadhaa kutokana na uwezo wake; ili uovu upambanuke kutokana na uzuri:

Miongoni mwa kuhuisha maiti atakayemuua.

Kudhihiri pambo la dunia na rutuba anayomiliki.

Pepo yake, moto wake na mito yake.

Kanzi za ardhi kumfuata yeye.

Na kuiamrisha kwake mbingu inyeshe na ardhi ioteshe.

Basi awe na uwezo wote huo kwa kuwezeshwa na Allah na kutaka kwake, kisha baada ya hapo Allah amyime uwezo, kama alivyosema [Mtume]: (na asiwezeshwe juu ya mwengine), basi asiwezeshwe tena kumuuwa yule mtu, wala mwengine, na hali yake ibatilike baada ya hapo, na Isa salamu zimshukie amuuwe, na Allah awathibitishe wale walioamini.

Huu ndio (ufahamu wa) mfumo wa ahlu ssunnah na mjumuiko wa watu wa fiq-hi na hadith na mfano wao"[1].

❉❉❉

1 Ikmaal Al-Mu'lim bi fawaaidi muslim (8/474).

## UDHAIFU WA DAJALI

Masihi dajali ni mtu dhaifu, hawezi kujiondolea ubovu wa jicho lake, na Muumini atakapodiriki masiku yake [yaani: ya kutoka kwake] ajikinge na Allah, na wala hatomdhuru chochote.

Al-Mudh-hiry Allah amrehemu amesema akinukuu imamu Abu Bakr Al-Kallaabaadhi (amekufa: 384 hijria) Allah amrehemu: "Na lau asingekuwa A’war na macho yake yakawa sawa hangekuwa akitatiza, lakini [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie ametaka kubainisha: ya kuwa yeye [Dajali] ni mtu wala si mnyama wala shetani.

Wala hana nguvu za zaidi wala hali ya ziada ya kuogopewa kuliko kuogopewa kiongozi wa watu dhalimu, mwenye nguvu na jabari.

Na kuwa yeye ni mtu mwili wake umefanana na miili yao, inamuuma kinacho wauma, na anahitajia yale wanayohitajia watu.

Na kuwa yeye amesibiwa na maafa ya ubovu wa jicho, hana uwezo wa kujiondolea nafsi yake ubovu huyo.

Lau Allah akimsalitishia mbu basi atamshughulisha na amuepushe na yote anayoyadai.

Na lau atautaharakisha mshipa wake uliokuwa umetulia, au akautuliza uliokuwa unataharaki nguvu zake zote zitapotea, na hali yake itamhofisha.

Basi [bayana] hii kutoka kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ni kumshajiisha yule atakayetahiniwa na masiku yake na kudiriki ufalme wake; ili hofu yake kumuogopa yeye isiwe

kubwa kuliko kumuogopa mmoja kati ya watu ambaye ana uwezo juu yake"[1].

Al-Mudh-hiry Allah amrehemu amesema: "Na upeo wa tafsiri ya Al-Kallaabaadhi: Ni kuwa Dajali ni mtu mfano wenu; bali ni dhaifu zaidi kuliko nyinyi; sababu yeye ni mbovu wa jicho, ubovu ni upungufu na aibu, basi yalazimu asiwe mwabudiwa kwa njia mbili:

Mojawapo: Ni kuwa mwabudiwa ni wajibu dhati yake isalimike kutokana na maafa na mapungufu.

Na ya pili: Ni kuwa lau angekuwa mwabudiwa basi angejiondolea aibu ya nafsi yake, wala hangeridhia nafsi yake upungufu.

Kisha ubovu wa jicho lake ukiwa ni kutokana na nafsi yake, basi mwabudiwa sifa zake hazipungui.

Na ukiwa ni kutokana na mwengine - nayo ndio hakika - basi yeye ni kiumbe mpungufu.

Basi inalazimu awe kama viumbe wengine waliosalia waliojeuri madhalimu"[2].

❋❋❋

1 Al-Mafaatiih fii sharhil maswaabiih (5/410).

2 Al-Mafaatiih fii sharhil maswaabiih (5/410).

## HALI YA MASIHI DAJALI HIVI SASA

Imekuja katika sunnah ya Nabii bayana ya hali ya Masihi dajali [alivyo] hivi sasa, na hali yake ni kama ifuatavyo:

1- Kuwa yupo hai sasa.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema - akieleza aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie kuhusi Dajali -: ((**Na mimi**[1] **nitawaeleza habari ya kunihusu, hakika mimi ni Masihi [dajali], na imekurubia nipewe idhini ya kutoka**)), imepokewa na Muslim.

2. Yupo katika kisiwa miongoni mwa visiwa vya bahari.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema - akieleza aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie kuhusi dajali -: ((**Amenihadithia kuwa amepanda jahazi pamoja na watu thelathini kutoka kabila la Lakhmi na Judhaam** [2]**, basi bahari ikawarusharusha mwezi, kisha wakakurubia kisiwa katika bahari hadi jua likachwa, basi wakakaa katika vijidau vya jahazi na wakaingia katika kisiwa**)), imepokewa na Muslim.

3. Amefungwa kwa kifungo kigumu cha chuma, na sifa ya hilo:

a- Mikono yake imekusanywa katika shingo yake na imefungwa na chuma.

b. Baina ya magoti yake hadi visiginoni mwake pia amefungwa na chuma.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie

1 Yaani: Masihi dajali.

2 **Lakhmi na Judhaam**: Kabila mbili kutoka Yemen.

amesema - akieleza aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie kuhusi Dajali -: (**Tukaondoka mbio hadi tukaingia katika kasri, mara tu tukaona ndani yake kuna mtu mwenye maumbile mkubwa sana hatujawahi kuona, amefungwa vigumu sana, mikono yake imekusanywa katika shingo yake, na kufungwa kwa chuma baina ya magoti yake hadi katika visigino vyake**), imepokewa na Muslim[1].

❉❉❉

1 Muslim, nambari (2942), miongoni mwa hadithi za Fatwima binti Qays Allah amridhie.

## ALAMA ZA KUTOKA KWA DAJALI

Zimekuja hadithi kutaja alama za kutoka kwa Masihi dajali, nazo:

1. Kuwa mitende ya Baysaan haitozaa.

Baysaan: Ni mji uliyo kaskazini ya Palestina, na kusini mwa ziwa la Twabariyyah, iko mbali nalo kwa (25) km, iko na umbali wa (120) km kutoka Baytul Maqdis.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema - akieleza aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie: ((**Basi akasema - yaani: Dajali -: Nielezeni kuhusu mitende ya Baysaan.**

**Tukasema: Habari yake gani unaulizia?**

**Akasema: Nawauliza kuhusu mitende yake, je inazaa? Tukasema: Ndio.**

**Akasema: Hakika imekurubia kutozaa**)), imepokewa na Muslim.

Na alama hii imeanza kudhiri kabla ya takriban miaka mia nane, Yaquut Al-Hamawi Allah amrehemu ((amekufa: 626 hijria) amesema: "Na nimeiona mara kadhaa; basi sikuona mitende ambayo haikuzaa isipokuwa miwili"[1].

1 Mu'jamul Buldaan (1/527).





2- Kuisha kwa maji ya ziwa la Twabariyyah.

Na maji yake sasa hivi yamepungua, na yanaendelea kupungua.

Na ziwa la Twabariyyah: lipo kaskazini mwa Palestina, karibu na Jaulaan, iko mbali na Baytul Maqdis kwa (150) km, nayo ni kaskazini mwa Baysaan, iko mbali nayo kwa (25) km.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: - akisimulia aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie -: ((**Akasema** - yaani: Masihi dajali -: **Nielezeni kuhusu ziwa la Twabariyyah.**

**Tukasema: Habari yake gani unaulizia?**


**Akasema: Je liko na maji?**

**Wakasema: Limejaa maji.**

**Akasema: Hakika maji yake yamekurubia kuisha**)), imepokewa na Muslim.


Acre
Haifa
ziwa la
Twabariyyah
Nazareth
Baysaan
[Beit She'an]
Irbid
Netanya
Jaffa
Adwaffatul Gharbiyyah
Baytil Maqdis
[Jerusalem]

# [Ziwa la Twabariyyah]







**[Ziwa la Twabariyyah; na inadhihiri ndani yake upungufu wa maji]**

3. Kuisha kwa maji ya chemchemi ya Zughar, na watu wake wasilime kwa (kutumia) maji yake.

Na chemchemi ya Zughar: Iko Jordan katika ufuo wa kusini mashariki mwa bahari Maiti, katika (bonde la As-Swaafy), karibu na [maji ya] maporomoko ya bonde la Al-Hasaa, iko mbali na Al-Karak kwa (27) km, na iko mbali na Baytul Maqdis kwa (85) km.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema - akisimulia aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie -: ((**Akasema** - yaani: Dajali -: **Nielezeni kuhusu chemchemi ya Zughar.**

**Tukasema: Habari yake gani unaulizia?**

**Akasema: Je mna maji katikika chemchemi? Na je watu wake wanalima kwa maji yake?**

**Tuakasema: Ndio, imejaa maji, na watu wake wanalima kutokana na maji yake**)), imepokewa na Muslim.

Abdul-Haqq Ad-Dahlawy (amekufa 1052 hijria) Allah amrehemu anasema: "Zughar: Ni kijiji kilichoko Shaam [Sirya], na ndani yake mnao chemchemi, kuisha kwa maji yake ni alama ya kutoka kwa Dajali"[(1)].

Na Muhammad Al-Bash-shaari [amekufa: 380 hijria] Allah amrehemu ameuelezea mji wa Zughar kwa kauli yake: "Ni mji wenye kuuwa wageni, maji yake ni machafu, na ambaye Malaika wa mauti atachelewa kumfikia basi auendee [mji huo] wala sijui mfano wake katika Uisilamu katika mlango huu, na hakika nimeona miji na [sehemu] zenye majanga lakini si kama sehemu hii[(2)]".

Na tulimkalifisha mmoja wetu mwenye kuaminika kusafiri


1 Lama'atu ttanqiih fii mishkaatil maswaqbiih (8/714).

2 Ahsanu ttaqaasiim fii ma'rifatil aqaaliim (uk. 178).

kuenda mji wa Zughar, na kuuliza watu wake kuhusu chemchemi ya Zughar; basi wakamuelekeza, na akaipiga picha na video chemchemi hio, na wenyeji wakamfahamisha: "kuwa kabla ya miaka kumi chemchemi ya Zughar ilikuwa imejaa maji matamu, na walikuwa wanyoshea mimea yao, na mategemeo yao yalikuwa juu yake.

Ama sasa mwaka wa (1443 hijria) maji yake ni machache sana; nao wanaiita (chemchemi ya 'Abaatwa)"[1].

1 Hayo maelezo yao yamethibitishwa kwangu kwa sauti na picha.


Jaffa
Adwaffatul Gharbiyyah
Baytil Maqdis
Jerusalem]
Bahari Maiti
Kerak
Mu'tah
Chemchemi ya Zughar
At-Tafilah





**[Chemchemi ya Zughar; na inadhihiri upungufu wa maji ndani yake]**

❋ **Na bayana ya hadithi zilizokuja katika hilo ni yanayofuata:**

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema - akieleza aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie kuhusi Dajali -: ((**Tukaondoka mbio hadi tukaingia katika kasri, mara tu tukaona ndani yake kuna mtu mwenye maumbile makubwa sana hatujawahi kuona, amefungwa vigumu sana, mikono yake imekusanywa katika shingo yake, na kufungwa kwa chuma baina ya magoti yake hadi katika visigino vyake.**

**Tukasema: Ole wako, ni nani wewe?**

**Akasema: Hakika mumeweza kuifikia habari yangu, basi nielezeni ni nani nyinyi?**

**Tukasema: Sisi ni watu katika waarabu, tulipanda jahazi, na tukasadifu wakati bahari imechafuka, basi mawimbi yakatuchezesha chezesha mwezi.**

**Kisha tukakurubia kisiwa chako hichi, tukakaa katika vidau na tukaingia katika kisiwa, tukakutana na mnyama mwenye nywele nyingi ngumu** - na katika mapokezi mengine: **mtu anakokota nywele zake -, hatambulikani mbele yake wala nyuma yake kwa wingi wa nywele.**

**Basi tukasema: Ole wako, ni nani wewe?**

**Akasema: Mimi ni Al-Jassaasa.**

**Tukasema: Na ni nini [Al-Jassaasa] jasusi [1]?**

**Akasema: Nendeni kwa mtu huyu ndani ya kasri, kwani yeye ni mwenye shauku mno wa habari zenu.**

**Basi tukakabili kukuijia na tukamuogopa, wala hatukuwa**

1 **[Al-Jassaasa] jasusi**: Ameitwa hivyo kwa sababu anajasusi habari kumpelekea Dajali.

**na utulivu asije akawa ni shetani.**

**Basi akasema: Nielezeni kuhusu mitende ya Baysaan.**

**Tukasema: Habari yake gani unaulizia?**

**Akasema: Nawauliza kuhusu mitende yake, je inazaa? Tukasema: Ndio.**

**Akasema: Hakika imekurubia kutozaa**

**Akasema: Nielezeni kuhusu ziwa la Twabariyyah.**

**Tukasema: Habari yake gani unaulizia?**

**Akasema: Je liko na maji?**

**Wakasema: Limejaa maji.**

**Akasema: Hakika maji yake yamekurubia kuisha.**

**Akasema: Nielezeni kuhusu chemchemi ya Zughar.**

**Tukasema: Habari yake gani unaulizia?**

**Akasema: Je mna maji katikika chemchemi? Na je watu wake wanalima kwa maji yake?**

**Tuakasema: Ndio, limejaa maji, na watu wake wanalima kutokana na maji yake),** imepokewa na Muslim[1].

❉❉❉

1 Muslim, nambari (2942), miongoni mwa hadithi za Fatwima binti Qays Allah amridhie.

## LINI ATATOKA MASIHI DAJALI?

Dajali amejitolea habari ya nafsi yake kuwa kutoka kwake kumekurubia, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akakiri hilo - akisimulia aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie kuhusu Dajali: ((**Nami**[1] **nitawapeni habari yangu; hakika mimi ni masihi [dajali], na hakika nimekurubia nipewe idhini yakutoka**)), imepokewa na Muslim[2].

Na ni katika alama za kutoka kwake: Kufutahiwa mji wa Konstantinopoli[3], wala si kuupiga vitu tu bila ya kuufutahi.

Waislamu wameupiga vita mara kadhaa, na vita vya kwanza vilikuwa katika kipindi cha Muawiya ibnu Abii Sufyan Allah awaridhie, mwaka (49 hijria), lakini haukufutahiwa.

Ama kufutahiwa kwake basi ni mara mbili:

Mara ya kwanza: Aliufutahi Muhammad ibnu Muraad ibnu Muhammad Allah amrehemu, anayeitwa (Muhammad Al-Faatih), mwaka (857 hijria) kwa vita, na futahi hii si alama ya kutoka kwa Dajali, kwa sababu ilikua futahi kwa kupitia vita.

Al-Mullaa Al-Qaary (1014 hijria) Allah amrehemu anasema: "Konstantinopoli: inafutahiwa kwa vita vingi"[4].

Na mara ya pili: itafutahiwa mwisho wa zama kwa [Tahliili] kauli ya 'Laa ilaaha illa llaah' na Takbiri bila ya vita, na futahi hii ni alama ya kutoka kwa Dajali.

Na pindi Waislamu wataifutahi Konstantinopoli mwishoni

---

1 Yaani: Masihi dajali.

2 Muslim, nambari (2942), miongoni mwa hadithi za Fatwima binti Qays Allah amridhie.

3 **Konstantinopoli**: Hivi sasa ni (Istanbul).

4 Mirqaatul mafaatiih (8/3416).

mwa zawa kwa Tahlili na Takbiri bila ya vita basi Masihi dajali atatoka, na zimejulisha hilo [hadithi] zinazofuata:

1. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Mushausikia mji ambao upande mmoja wake uko katika bara**[1] **na upande mwingine katika maji**[2]**?**

Wakasema: Naam, ewe Mtume wa Allah.

Akasema: **Hakisimami Kiyama hadi watu elfu sabiini kutoka wana wa Is-haaq**[3] **waupige vita [mji huo]**.

**Basi watakapouijia watashuka, hawatapigana kwa silaha wala hawatarusha mshale, watasema: 'Laa ilaaha illa llaah wa llaahu akbar', basi uanguke mmoja wa pande zake mbili**[4]**,** - Thawr anasema: Sijui ila kuwa amesema: ambao uko baharini[5].

**Kisha waseme: 'Laa ilaaha illa llaah wa llaahu akbar', basi wafarajiwe, na wauingie na wakusanye ngawira.**

**Basi wakati wao wako katika hali ya kugawanya ngawira, mara tu uwaijie ukelele**[6]**, usema: Hakika Dajali ametoka, basi waache kila kitu na warudi**), imepokewa na Muslim[7].

2. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Na waufutahi**[8] **mji wa Konstantinopoli, Basi wakati wao wako katika hali ya kugawanya ngawira wakiwa**

1 Nao ni upande wake wa mashariki na wa magharibi.

2 Nao ni upande wake wa kaskazini na wa kusini.

3 **Wana wa Is-haaq**: yaani katika kizazi cha Nabii Is-haaq salamu zimshukie, nao ni waisilamu.

4 **mmoja wa pande zake mbili**: yaani: upande mmoja wa ngome ya mji.

5 **ambo uko baharini:** yaani: upande wake ambao uko baharini.

6 **ukulele**: Sauti ya mwenye kutaka uokozi.

7 Muslim, nambari (2920).

8 Yaani: Waisilamu.

**wametungika panga zao katika mti wa zeituni, mara tu shetani apige ukelele kati yao: Hakika Masihi [Dajali] nyuma yenu amevamia watu wenu, basi watoke, na hilo ni batili.**

**Basi watakapofika [Shaam] Sirya [Dajali] atatoka**)), imepokewa na Muslim[1].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Ataidhinishwa - yaani: Dajali - kutoka katika zama za mwisho, baada ya waisilamu watakapofutahi mji wa waroma unaoitwa: Konstantinopoli"[2].

1 Muslim, nambari (2897).

2 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/205).

## SABABU YA KUTOKA MASIHI DAJALI

Allah amejaalia kuwa kila kitu kiko na sababu; na sababu ya kutoka kwa Dajali ni kutokana na ghadhabu atakayoghadhibika, Naafi' Allah amridhie amesema: Ibnu Umar alikutana na ibnu Swaaid katika baadhi ya njia za Madina, akamwambia neno likamghadhibisha, basi akafura kwa hasira hadi akajaa katika njia.

Basi ibnu Umar akaingia kwa Hafswa [mke wa Mtume] na akamueleza.

[Hafswa] akamwambia: Allah akurehemu, umetaka nini kutoka kwa ibnu Swaaid?! Kwani hakujua kuwa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika [Dajali] atatoka kwa sababu ya ghadhabu atakayo ghadhibika nayo**)), imepokewa na Muslim[1].

As-Swan'ani (amekufa: 1182 hijria) Allah amrehemu amesema: "Wala hakutaja sababu yake [ghadhabu hiyo], na makusudio: Ni kuwa Allah aliyetukuka atakapokadiria kutoka kwake atasababisha kughadhibika kwake"[2].

❊❊❊

1 Muslim, nambari (2932).

2 At-Tanwiiru sharhul jaamiu sswaghiir (4/205).

## SEHEMU ATAKAYOTEKEA MASIHI DAJALI

Sunnah ya Nabii imekuja kubainisha sehemu atakayotoka Masihi dajali, na ubainifu wa hilo ni katika yanayofuata:

1. Kuwa atatoka upande wa mashariki, yaani: mashariki ya Madinah.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika yeye yupo katika bahari ya Shaam [1], au bahari ya Yeman [2], hapana, bali kutoka upande wa mashariki** [3])), imepokewa na Muslim[4].

2. Abu Abdillah Muhammad Al-Qurtuby Allah amrehemu amesema: “Ni shaka au dhana kutoka kwake Mtume swala na salamu zimshukie, au amekusudia kumficha anayesikia, kisha akakanusha hilo, na akayafuta kwa kutaja hakika, akasema: (hapana, bali ni kutoka upande wa mashariki)”[5].

❉❉❉

1 **Bahari ya Shaam**: ni bahari nyeupe ya katikati.

2 **Bahari ya Yemen**: iko kusini mwa Yemen na Oman, na leo hii inaitwa: (Bahari Arabu).

3 Sifa hii inalingana na (bahari ya Qazwiin), nayo ni bahari kubwa zaidi inayozungukwa na bara kavu katika pande zake zote.

4 Muslim, nambari (2942).

5 At-Tadhkira bi ahwaalil mautaa wa umuuril aakhira (uk 1344).


Uturuki
Armenia
Azerbaijan
Baku
Bahari ya mashariki
Cyprus
Syria
Bahari ya Mediterania
Jerusalem
Jordan
Iraq
Irani
Kuwait
Ghuba ya uarabuni
Bahreni
Madinah Al-Munawwarah
Katari
Saudia
jeddah
Makkah tukufu
bahari nyekundu
Eritrea
Yemen

3- Atatoka Khorasan.

Na Khorasan: Ni mkoa mkunjufu, unakusanya: kusini mwa bahari ya Qazwiin, kusini magharibi yake, na kusini mashariki yake, pamoja na kukunjuka kwake upande wa kusini[1].

Abu Bakr As-Swidiiq Allah amridhie amesema: ((Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie ametuhadithia: **Kuwa Dajali atatoka katika ardhi ya mashariki, inaitwa: Khuraasaan, watamfuata yeye watu kana kwamba nyuso zao ni ngao zilizogongwa**[2])), imepokewa na Ahmad. [3]"

❊❊❊

---

1 Mipaka ya Khuraasaan/Khorasan: kaskazini kuna bahari ya Qazwiin, na mto wa Jayhuun, na kusini: kuna Kerman, na mashariki mna Kabul, na magharibi kuma Junaqan.

2 Zilizogongwa: Ambazo zimegongwa baadhi yake juu ya nyengine, An-Nawawy Allah amrehemu amesema katika sherehe ya Muslim (18/37): "Na maana yake ni kufananisha nyuso za waturuki katoka upana wake na nyuso zo na kufura kwa mashavu yao na ngao zilizobondwa".

3 Musnad, nambari (12).


Khawaarizm
Uzbekistan
Bahari ya mashariki
Azerbaijan
Mto wa Jiihuun
Ardabil
Turkmenistan
Khorasan
Kabul
Afghanistam
Junaqan
Irani
Kerman
Omani

4- Watamfuata yeye mayahudi wa Asbahaan (Isfahan) elfu sabiini, wakiwa wamevaa [Twayaalisah] vazi la kiyahudi.

Na Asbahaan (Isfahan): Ni mji ulio kusini mwa Tehran, uko mbali nao kwa (450) km.

Na Twayaalisah: Ni aina ya nguo, mayahudi wanajifunika nayo vichwa vyao au mabega yao.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Watamfuata Dajali mayahudi elfu sabiini wa Asbahaan, wakiwa wamevaa [Twayaalisah] vazi la kiyahudi**)), imepokewa na Muslim[1].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Mwanzo wa kudhihiri kwake ni kutoka Asbahaan (Isfahan), katika mtaa unaoitwa (Al-Yahuudiyyah), na watamnusuru yeye katika watu wa mji huo mayahudi elfu sabiini, wakiwa na silaha na [Siijaan] - nayo ni Twayaalisah za kijani -, vilevile atanusuriwa na watu elfu sabiini kutoka Tatars, na wengine katika watu wa Khorasan"[2].

❉❉❉

1 Muslim, nambari (2944).

2 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/205).


Azerbaijan
Baku
Bahari ya mashariki
Ardabil
Zanjan
Sariyer
Qazwiin
Sanandaj
Kermanshah
Araak
[mti wa msuwaki]
Kashan
Isfahan





**Twayaalisah**

5. Atakapotoka itakuwa hamu yake na malengo yake ni Madinah.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Dajali atakuja kutokea upande wa mashariki, yatakuwa malengo yake ni Madinah**)), imepokewa na Muslim[1].

Na huenda sababu ya yeye kukusudia Madinah; ni kuwa zama za mwisho imani itarudi huko [Madinah], Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika imani itarudi Madinah kama vile nyoka anavyorudi katika shimo lake**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[2].

6- Ataenda madinah kupitia njia iliyo baina ya Shaam na Iraq.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atatoka katika. njia baina ya Shaam na Iraq**)), imepokewa na Muslim[3].

Abul Abbaas Ahmad Al-Qurtuby (amekufa: 656 hijria) Allah amrehemu: "Mwanzo wa kutoka kwa Dajali ni kutoka Khorasan, kisha atatoka kuelekea Hijazi kupitia baina ya Iraq na Shaam"[4].

❊❊❊

1 Muslim, nambari (1380).

2 Bukhari, nambari (1876), na Muslim, nambari (147), miongoni mwa hadithi za Abu Hureira Allah amridhie.

3 Muslim, nambari (147), miongoni mwa hadithi za An-Nawwaas ibnu Sam'an Allah amridhie.

4 Al-Mufhim limaa ashkala min talkhiis kitaabi muslim (23/116).



Bahari ya Qazwiin
Kuwait
Ghuba ya uarabuni
Bahrain
Madinah
Saudia

## HALI YA WATU PINDI ATAKAPOTOKA MASIHI DAJALI

Sunnah ya Nabii imekuja kubainisha hali ya watu pindi atakapotoka Masihi dajali, nayo ni kama ifuatayvo:

1- Kuwa wao watamkimbia na kuelekea majabalini. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika watu watamkimbia Dajali katika majabali**)), imepokewa na Muslim.

2- Waisilamu watakuwa katika vita na waroma, kisha waisilamu watanusurika juu yao na wapate ngawira, mara waisikie kutoka kwa Dajali, basi watupe ngawira na mali yaliyo mikononi mwao; ili kukimbilia kuwanusuru wanawake wao na watoto wao, wanarudia watu huku wakijulia habari yake.

Ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: "Wakati wao wako kwenye hali hiyo mara tu watasikia janga ambalo ni kubwa kuliko hilo (walionalo), utawaijia ukelele: Dajali nyuma yenu amewavamia katika wake zao na watoto wao.

Basi watupe yalio mikononi mwao, na waelekee huko, watume watu kumi [waliopanda farasi] wakaangalie hali yake [Dajali]", imepokewa na Muslim.

3- Atakapowasili Madinah atatoka mtu muumini miongoni mwa watu wa Madinah kumwendea, na amwambie: Nashuhudia kuwa wewe ni Dajali.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: (Basi siku hiyo atamtokea mtu ambaye ni mbora wa watu - au: miongoni mwa wabora wa watu -, na amwambie: Nashuhudia kuwa wewe ni Dajali), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

❋ **Bayana ya hadithi zilizokuja katika hilo ni kama ifuatavyo:**

Amepokewa Ummu Shariik Allah amridhie: ((Kuwa amemsikia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akisema: **Watu watamkimbia Dajali [waelekee] majabalini.**

Ummu Shariik akasema: Ewe Mtume wa Allah, waarabu siku hio watakuwa wapi?

Akasema: **Wao ni wachache**)), imepokewa na Muslim[1].

Amepokea Yusayr ibnu Jaabir kuwa Abdallah ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: ((Kiyama hakitasimama hadi mirathi iache kugawanywa, wala ngawira isifurahikiwe, kisha akaashiria na mkono wake hivi - na akaueleza upande wa Shaam, na akasema: Maadui watakusanyika dhidi ya Waisilamu, na Waislamu watakusanyika dhidi yao.

Nikasema: Unawakusidia waroma?

Aksema: Ndio; na katika vita hivyo kutakuwa na majibizano makali.

Basi Waislamu waandae kikundi cha kupigana hadi kufa, hakirudi ila na ushindi, wapigane hadi usiku uwazuie baina yao, basi hawa warudi na hawa warudi, wote hawakushinda, na kikundi kiishe.

Kisha Waislamu waandae kikundi [chengine] cha kupigana hadi kufa, hakirudi ila na ushindi, wapigane hadi usiku uwazuie baina yao, basi hawa warudi na hawa warudi, wote hawakushinda, na kikundi kiishe.

Waislamu waandae kikundi [chengine] cha kupigana hadi kufa, hakirudi ila na ushindi, wapigane hadi jioni, basi hawa

1 Muslim, nambari (2945).

warudi na hawa warudi, wote hawakushinda, na kikundi kiishe.

Basi itakapofika siku ya nne; Waislamu waliosalia [wote] watawainukia, basi Allah atajaalia kushindwa ni juu yao [jeshi la Dajali], na wauliwe kuuliwa - ima alisema: hakutaonekana mfano wake, na ima alisema: hakujaonekana mfano wake -, hadi ndege akipita ubavuni mwao hatawavuka isipokuwa ataanguka akiwa maiti, basi watoto wa baba mmoja waliokuwa mia moja wajihisabu na wasijikute ila wamebakia mmoja tu, basi ni ngawira gani itafurahiwa?! Na ni urathi gani utagawanywa?!

Basi wakiwa katika hali hiyo mara tu wasikie janga kubwa zaidi kuliko hilo, uwaijie ukelele: Dajali nyuma yao amevamia wanawake na watoto wao.

Basi watupe yaliyomo mikononi mwao, waelekee huko na watume watu wapiganaji kumi walio juu ya farasi kuwajulia habari [hiyo].

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: **Hakika mimi nawajua majina yao, majina ya baba zao, na rangi za farasi wao.**

**Wao ni wapiganaji bora zaidi juu ya mgongo wa ardhi siku hio** - au: **ni miongoni mwa wapiganaji bora zaidi juu ya mgongo wa ardhi siku hio** -)), imepokewa na Muslim[1].

Na kauli ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika hadithi: ((**Hakika mimi nawajua majina yao, majina ya baba zao, na rangi za farasi wao**)), na kauli yake katika hadithi nyengine: ((**Basi wakati wao wako katika hali ya kugawanya ngawira wakiwa wametungika panga zao katika mti wa**

1 Muslim, nambari (2899).

**zeituni**))[1], inajulisha ya kuwa vita katika mwisho wa zama vitakuwa juu ya farasi na kwa panga.

Na je [vita] vitakuwa kwa hayo mawili peke yake au pamoja na njia za kivita za kileo?

Hakuna ajuaye hilo isipokuwa Allah.

3- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atatoka Dajali basi mmoja kati ya waumini amwendee, basi likutane naye jeshi - la Dajali – lenye silaha, wamwambie: Unaenda wapi?**

**Naye awajibu: Naeleke kwa huyu aliyetokeza.**

**Wamwambie: Hivi humwamini mola wetu mlezi?**

**Aseme: Mola wetu hana kufichika.**

**Basi waseme: Muuweni.**

**Waambiane baadhi yao kwa baadhi: Si mola wenu amewakataza kumuuwa yeyote bila yeye (kujua au kuwapa idhini)?**

**Waende naye kwa Dajali, basi yule muumini akimuona Dajali atasema: Enyi watu, huyu ni Dajali yule ambaye Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amemtaja.**

**Basi Dajali aamrishe alazwe kifudifudi.**

**Aseme: mchukueni na mumjuruhi kichwa, basi mgongo wake na tumbo lake yaenee kichapo.**

**Aseme: Bado hivi huniamini mimi?**

**Aseme: Wewe ndiye Masihi muongo.**

**Aamrishe achukuliwe na apasuliwe kwa msumeo kutoka**

1 Imetangulia takhriji yake,

**katikati ya mwili wake ili agawanywe baina ya miguu yake, kisha Dajali atembee baina ya vipande viwili, kisha aseme: Simama, basi astawi akiwa amesimama.**

**Kisha amwambie: Je utaniamini?**

**Aseme: Sijazidi ila kukutambua (kwa yakini), kisha aseme: Enyi watu, hakika yeye [Dajali] hawezi kumfanya yeyote baada yangu.**

**Basi Dajali amchukue ili amchinje, basi baina ya shingo yake hadi mfupa wa mabega yake itakuwa shaba, na asiweze [kumchinja], basi amshike mikono yake na miguu yake amrushe, watu watadhania amemtupa motoni, na hakika ametiwa peponi.**

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: **Huyu ndiye mtu aliye na ushahidi mkubwa zaidi mbele ya Mola Mlezi wa viumbe wote**)), imepokewa na Muslim[(1)].

4- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema - kumhusu Dajali - : ((**Basi afike katika baadhi ya ardhi maiti [ardhi isiomea kitu kwa ajili ya kuwa na chumvi] ambayo imekurubia Madinah, basi amtokee siku hiyo mtu aliye mbora zaidi - au miongoni mwa watu bora zaidi - na amwambie: Nashuhudia kuwa wewe ni Dajali ambaye Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie ametuhadithia habari yake.**

**Basi Dajali aseme: Mwaonaje lau nitamuuwa huyu kisha nimhuishe; je mtashuku katika amri yangu?**

**Wasema: Hapana, basi amuuwe kisha amhuishe.**

**Basi asema [yule mtu] pindi [Dajali] atamhuisha: Naapa**

1 Muslim, nambari (2938).

**kwa Allah sijakuwa na elimu zaidi kukuhusu zaidi nilivyonayo sasa.**

**Basi dajali atake kumuuwa wala asiwezeshwe**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

❉❉❉

1 Bukhari, nambari (7132), na Muslim, nambari (2938), miongoni mwa hadithi za Abu Said Al-Khudry Allah amridhie.

## MWENDO WA KASI WA MASIHI DAJALI KATIKA ARDHI.

1- Mwendo wa Masihi dajali katika ardhi ni wa kasi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amefananisha mwendo wake wa kasi na mwendo wa kasi wa mvua inaposukumwa na upepo.

An-Nawwaas ibnu Sam'aan Allah amridhie amesema: ((Tukasema: Ewe Mtume wa Allah, ni vipi kasi yake[1] juu ya ardhi? Akasema: **Kama mvua inayosukumwa na upepo**)), imepokewa na Muslim[2].

2- Katika kutembea kwake kwa kasi juu ya ardhi: ni hataacha kijiji ila atakiingia ndani ya siku arubaini isipokuwa Makkah na Madinah, kwani miji hiyo miwili ameharamishiwa.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie - akisimulia aliyoyasema Tamiim Ad-Daary Allah amridhie kuhusi Dajali -: ((**Na mimi**[3] **nitawapa habari yangu; mimi ndiye Masihi [Dajali].**

**Na mimi imekurubia niidhinishwe kutoka, nitoke na nitembee katika ardhi, basi sitaacha kijiji ila nitakiingia katika siku arubaini, isipokuwa Makkah na Madinah, kwani miji hiyo miwili nimeharamishiwa.**

**Kila nikitaka kuingia mojawapo ya hizo mbili; Malaika ananikabili akiwa na upanga uliochomolewa mkononi mwake, ananizuilia kuingia, na katika kila mlango miongoni mwa**

1 Yaani: Masihi dajali.

2 Muslim, nambari (2937).

3 Yaani: Masihi dajali.

**milango yake mna Malaika wanaulinda**)), imepokewa na Muslim[1].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Na atakurubia na aingie miji; kijiji kwa kijiji, ngome kwa ngome, mkowa kwa mkowa, na mji kwa mji, na wala hakutabakia mji katika ya miji ila ataukanyaga na jeshi lake lenye farasi na linalotembea [yaani: kwa uwezo wake wote], isipokuwa Makkah na Madinah"[2].

❉❉❉

1 Muslim, nambari (2937).

2 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/205).

## MASIHI DAJALI HATOINGIA MAKKAH WALA MADINAH

Masihi dajali atatembea juu ya ardhi na aiingie miji yake ila Makkah na Madinah, kwani hiyo ni miji miwili adhimu, Allah amemuharamishia kuyaingia.

❋ **Na bayana ya hadithi katika hilo ni kama ifuatavyo:**

1- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakuna mji wowote ila Dajali atauingia, isipokuwa Makkah na Madinah, na hakuna njia katika njia zake [za kuingia] ila kuna Malaika wamepanga safu wanailinda**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

2- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika Madinah imezungukwa na Malaika, katika kila mlango wake kuna Malaika wawili wanaulinda, Tauni haingii wala Dajali.**

**Atakayeikusudia na uovu Allah atamyayusha kama inavyoyayuka chumvi ndani ya maji**)), imepokewa na Ahmad[2].

3- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Juu ya milango ya Madinah mna Malaika, Tauni haiingii wala Dajali**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[3].

❋❋❋

1 Bukhari, nambari (1881), na Muslim, nambari (2943), miongoni mwa hadithi za Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

2 Al-Musnad, nambari (8373), miongoni mwa hadithi za Sa'd ibnu Maalik na Abu Hureira Allah awaridhie.

3 Bukhari, nambari (1880), na Muslim, nambari (1379), miongoni mwa hadithi za Abu Hureira Allah amridhie.

## MADINAH HAINGII NDANI YAKE HOFU YA MASIHI DAJALI

Miongoni mwa fadhila za Allah juu ya Waumini ndani ya Madinah ni kuwa Masihi dajali atakapotoka wao hawataingiwa na hofu wala hawatamuogopa, amepokewa Abu Bakrah Allah amridhie kutoka kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kuwa amesema: ((**Hofu ya Masihi dajali haitaingia Madinah, siku hiyo itakuwa na milango saba, juu ya kila mlango kuna Malaika wawili**)), imepokewa na Bukhari[1].

Na atakaposhukia Jurf - kando ya Madinah -, Madinah itatingisika mitingisiko mitatu, basi atoke kumwendea kila kafiri na mnafiki, Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atashukia**[2] **katika ardhi maiti** - na katika riwaya: **basi aje katika ardhi maiti ya Jurf** - **akitishe mahema yake, na Madinah itatingisika mitingisiko mitatu, basi atoke kumwendea kila kafiri na mnafiki**), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[3].

Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: "kauli yake (Kisha Madinah itingisike), yaani: itatokea zilzala baada ya nyengine, kisha [zilzala] ya tatu, hadi atoke kila asiyekuwa mwenye ikhlasi katika imani yake, na atabakia ndani yake muumini mwenye ikhlasi, wala Dajali asipewe uwezo juu yake.

Wala hili hapingani na yaliotajwa katika hadithi ya Abu Bakrah iliyotangulia kuwa (hofu ya Dajali haitaingia Madinah); kwa sababu makusudio ya hofu: Ni yatakayotokea miongoni mwa

1 Bukhari, nambari (1879).

2 Yaani: Masihi dajali.

3 Bukhari, nambari (1881), na Muslim, nambari (2943), miongoni mwa hadithi za Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

hofu ya kutajwa kwake, na hofu ya udhalimu wake, wala si hofu ya mtingisiko utakaopatokana kwa zilzala ili kuwatoa [Madinah] wasiokuwa na ikhlasi"[1].

Na Al-Kuuraany (amekufa: 893 hijria) Allah amrehemu amesema: "Na ukisema: Ikiwa hofu yake haitaingia Madinah, basi vipi watoke watu wa kufuru na unafiki?

Nitasema: Waliotoka wametoka kwa hofu ya zilzala, na kwa tamaa walionayo juu ya kupata pepo kheri alizonazo [Dajali]"[2].

❉❉❉

1 Fat-hul Baari (4/96)

2 Al-Kawthar al-Jaariy ilaa Riyaadhi Ahaadiith al-Bukhaariy (11/47).

## SEHEMU ATAKAYOSHUKIA MASIHI DAJALI KANDO YA MADINA

Pindi atakapotoka Dajali hamu yake na makusudio yake yatakuwa ni Madinah, wala hataweza kuiingia, wala kuingia Makkah, na ataingia miji ya ardhi yote, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakuna mji ispokuwa Dajali atauingia, ila Makkah na Madinah**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

Kisha atashukia kando ya Madinah, nje ya mipaka ya haram, katika Sabkhatul Jurf (ardhi maiti ya eneo la Jurf) nyuma ya jabali la Uhud, Kisha Malaika wataugeuza uso wake upande wa Shaam, na aangamie huko.

Na zimekuja hadithi kuelezea sehemu atakayoshukia Madina, nazo ni zifuatazo:

1- Atashukia kando ya Madinah, yaani: ubavuni mwake.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hadi ashukie kando ya Madinah**)), imepokewa na Bukhari.

2- Atashukia nyuma ya Uhud.

Na Uhud: Ni jabali kusini mwa Madinah, liko mbali na msikiti wa Nabii kwa (4) km.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hadi ashukie nyuma ya Uhud**)), imepokewa na Muslim.

1 Bukhari, nambari (1881), na Muslim, nambari (2943), miongoni mwa hadithi za Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

3- Atashukia katika [Sabkhatul Jurf] ardhi maiti ya Jurf.

Na Sabkhah: Ni ardhi isiomea kitu kwa ajili ya chumvu yake.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Basi aje katika [sabkhah] ardhi maiti ya Jurf**)), imepokewa na Muslim.

4- Kisha Malaika wageuze uso wake upande wa Shaam.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Kisha Malaika wataugeuza uso wake upande wa Shaam, na huko ndiko ataangamia**)), imepokewa na Muslim.

❉❉❉


Msitu
Ardhi mfo ya Jurf
Jabali la Uhud
Laayoune
Bwana wa Mashahidi
Kisima cha Uthmaan
Msikiti wa Dir'a
Wana wa Haaritha
Bendera
Al-Qiblatein
Fat-hi
Al-Maswaani'a
Al-Anaabis
Budhwa'a
Msikiti wa Nabii
Ar-Rab-wah
Qurbaan
Al-Jumu'ah


Adwaffatul Gharbiyyah
Mlango
wa Ludd [Lod]
Omani
Baytil Maqdis
[Jerusalem]
Jordan
Sakaka
Tabuk
Al-Ghardaqah
Al-Ulaa
Madinah
Yambu'a

❋ **Na bayana ya hadithi zilizokuja katika hilo ni kama ifuatavyo:**

1- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atakuja Dajali hadi ashukie kando ya Madinah, kisha Madinah itatingisika mitingisiko mitatu, basi atoke kumwendea kila kafiri na mnafiki**)), imepokewa na Bukhari[1].

2- Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atakuja Masihi [dajali] kutoka upande wa mashariki, hamu yake ni Madinah, hadi ashukie nyuma ya Uhud.**

**Kisha Malaika wataugeuza uso wake upande wa Shaam, na huko ndiko ataangamia**)), imepokewa na Muslim[2].

3- Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakuna mji wowote ila Dajali atauingia, isipokuwa Makkah na Madinah, wala hakuna mlango miongoni mwa milango yake ila juu yake wapo Malaika wamepiga safu, waulinda.**

**Basi ashukie katika Sabkhah (ardhi maiti)** - na katika riwaya ya Muslim: **basi aijie ardhi maiti ya Jurf na apige mahema yake** -, **na Madinah itingisike mitingisiko mitatu, watoke kumwendea kila kafiri na mnafiki**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[3].

❋❋❋

1 Bukhari, nambari (7124), miongoni mwa hadithi za Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

2 Muslim, nambari (1380), miongoni mwa hadithi za Abu Hureira Allah amridhie.

3 Bukhari, nambari (1881), na Muslim, nambari (2943), miongoni mwa hadithi za Anas ibnu Maalik Allah amridhie.

## MDA WA KUKAA MASIHI DAJALI KATIKA ARDHI

Kwa ajili ya ukubwa wa fitina ya Dajali masahaba walimuuliza Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kuhusu mda wa kubaki kwake katika ardhi; An-Nawwaas ibnu Sam'aan Allah amridhie amesema: ((Tulisema: Ewe Mtume wa Allah, na ni kiasi gani kukaa kwake ardhini?

Akasema: **Siku arobaini; siku moja ni kama mwaka, na siku moja ni kama mwezi, na siku moja ni kama wiki, na siku zake zilizosalia ni kama siku zenu.**

Tukasema: Ewe Mtume wa Allah, Hiyo siku ambayo ni kama mwaka; Je zitatutosheleza ndani yake swala za siku [yaani: swala tano tu]?

Akasema: **Hapana, ikadirieni kipimo chake**)), imepokewa na Muslim[1].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Na makadirio ya huo [mda wa Dajali ardhini]: ni mwaka na miezi miwili na nusu"[2].

❊❊❊

1 Muslim, nambari (2937).

2 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/205).

## FITINA YA MASIHI DAJALI

Anao Dajali fitina kubwa ambayo Allah atatahini nayo waja wake; kwa atakayoyaumba pamoja naye miongoni mwa mambo yanayotoka nje ya nidhamu ya kikawaida yatakayoonekana katika zama zake, na Allah atamuezesha vitu ambavyo ni katika uwezo wake.

Na katika hayo yanayotoka nje ya nidhamu ya kikawaida ni yanayofuata:

1- Anao mito miwili yanayotembea:

Mmojawapo: mwenye kuona anayaona kuwa ni maji meupe.

Na mwengine: mwenye kuona anayaona kuwa ni moto unaorurumba.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Mimi najua zaidi aliyonayo Dajali kuliko hata yeye mwenyewe, anao mito miwili inayotembea, mmojawapo kwa mtazamo wa jicho ni maji meupe, na mwengine kwa mtazamo wa jicho ni moto unaorurumba**)), imepokewa na Muslim.

2- Kuamrisha kwake mbingu inyeshe nayo inyeshe, na ardhi ioteshe nayo ioteshe.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Basi aiamrishe mbingu nayo inyeshe, na aiamrishe ardhi nayo ioteshe**)), imepokewa na Muslim.

3- Wale watakaomwamini na kumwitikia: ataamrisha mbingu iwanyeshee nayo itawanyeshea, na atamrisha ardhi iwaoteshee nayo itawaoteshea, na mifugo yao ilishe hadi ishibe na maziwa yao yakithiri.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Basi atawaijia watu na awalinganie nao**

**watamwamini na wamwitikie, basi aiamrishe mbingu nayo inyeshe, na ataamrisha ardhi nayo ioteshe, basi mifugo yao irudi jioni kutoka malishoni na hali nundo zao zimekuwa kubwa zaidi [kwa kunenepa], na ikiwa imejaa maziwa, na mbavu zilizofura**)), imepokewa na Muslim.

4- Wale ambayo hawatamwitikia na watakataa amri yake: watakumbwa na chaka na upungufu, na kufa kwa mifugo yao, na kupungukiwa na mali, nafsi na matunda.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Kisha atawaijia watu [wengine] na awalinganie, nao wakatae kauli yake, basi awaondokee, wapambazuke wakiwa ndani ya chake hawana mikononi mwao chochote katika mali yao**)), imepokewa na Muslim.

5- Kanzi za ardhi kumfuata, yaani: kanzi zilizozikwa au maadini za ardhi.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Na atapita katika magofu, na aseme kuiambia: Toa kanzi zako, basi kanzi zimfuate kama nyuki wanavyofuata mfalme wao**)), imepokewa na Muslim.

6- Atamhuisha maiti ambaye yeye ndiye amemua, kisha baada ya hapo Allah atamyima uwezo; basi asiweze kumuua mtu yule ambaye amemuhuisha baada ya kumuuwa wala mwengine.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Kisha amwite mtu barobaro, na ampige kwa upanga na amkate vipande viwili, [vuruke mbali mbali] baina yake ni umbali wa kurusha uta, kisha amwite na [asimame] aje na huku uso wake unamemetuka na anacheka**)), imepokewa na Muslim.

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "kwanza atadhihiri katika sura ya mfalme miongoni mwa wafalme majabari, kisha

atadi unabii, kisha atadai uola, basi wamfuate katika hilo wajinga wa binadamu, na watu duni na wasio na elimu, na atamhalufu na kumjibu yule atakayeongozwa na Allah miongoni mwa waja wake wema, na kundi la Allah wachamngu"[1].

Al-'Ainy (amekufa: 855 hijria) Allah amrehemu amesema: "Na faida ya kuwezeshwa na haya yenye kutoka katika nidhamu ya kikawaida: ni kuwatahini waja"[2].

1 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/205).

2 'Umdatul qaary sharhu swahiihil bukhaary (24/216).

❋ **Na bayana ya hadithi zilizokuja katika hilo ni kama ifuatavyo:**

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Hakika dajali anao pamoja naye pindi atakapotoka maji na moto.**

**Ama ule wanaouona watu kuwa ni motobasi ni maji baridi.**

**Na ama ule wanaouona watu kuwa ni maji baridi basi ni moto unaochoma.**

- Muslim amezidisha katika riwaya: **Basi msiangamie** -.

**Atakayekutana naye miongoni mwenu basi aingie katika ule anaouona kuwa ni moto, kwani huo ni [maji] tamu na baridi**, - na katika riwaya ya Muslim: **tamu mazuri** -), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

2- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Mimi najua zaidi aliyonayo dajali kuliko hata yeye mwenyewe, anao mito miwili inayotembea, mmojawapo kwa mtazamo wa jicho ni maji meupe, na mwengine kwa mtazamo wa jicho ni moto unaorurumba.**

**Basi pindi mmoja wenu atakutana naye aende katika mto anaouona kuwa ni moto, afunge macho yake, ainamishe kichwa chake na anywe, kwani hakika huyo ni maji baridi**)), imepokewa na Muslim[2].

3- Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Basi atawaijia watu na awalinganie nao**

---

1 Bukhari, nambari (3450), na Muslim, nambari (2935), miongoni mwa hadithi za Hudheifa ibnul yamaan Allah awaridhie.

2 Muslim, nambari (2934), miongoni mwa hadithi za Hudheifa ibnul yamaan Allah awaridhie.

**watamwamini na wamwitikie, basi aiamrishe mbingu nayo inyeshe, na ataamrisha ardhi nayo ioteshe, basi mifugo yao irudi jioni kutoka malishoni na hali nundo zao zimekuwa kubwa zaidi [kwa kunenepa], na ikiwa imejaa maziwa, na mbavu zilizofura, kisha atawaijia watu [wengine] na awalinganie, nao wakatae kauli yake, basi awaondokee, wapambazuke wakiwa ndani ya chake hawana mikononi mwao chochote katika mali yao, na atapita katika magofu, na aseme kuiambia: Toa kanzi zako, basi kanzi zimfuate kama nyuki wanavyofuata mfalme wao, Kisha amwite mtu barobaro, na ampige kwa upanga na amkate vipande viwili, [viruke mbali mbali] baina yake ni umbali wa kurusha uta, kisha amwite na [asimame] aje na huku uso wake unamemetuka na anacheka**), imepokewa na Muslim[1].

❉❉❉

1 Muslim, nambari (2937), miongoni mwa hadithi za An-Nawwaas ibnu Sam'an Allah awaridhie.

## HEKIMA KATIKA FITINA YA MASIHI DAJALI

Allah ataamrisha kutoka kwa Masihi dajali katika zama za mwisho kuwatahini waja; ili waumini wazidi imani kwa kuwa na yakini kwao juu ya urongo wa madai yake [Dajali] kuwa yeye mola, na ili makafiri na wale walio na maradhi ndani ya nyoyo zao wazidi shaka, ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Na Allah ameumba katika mikono yake [Dajali] mengi ya kutoka nje ya nidhamu ya kikawaida, anawapoteza kwayo anayemtaka katika waja wake na anawathibitisha kwayo waumini, basi wazidi kwayo imani pamoja na imani yao, na uongofu juu ya uongufu wao"[1].

Al-Mughirah ibnu Shu'bah Allah amridhie amesema: ((Hakuna yeyote alimuuliza Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kuhusu dajali zaidi kuliko nilivyomuuliza mimi, akasema: **Na ni lipi swali lako?**

Asema: Nikasema: wao wanasema [Dajali] anao pamoja naye majabali ya mkate na nyama, na mto wa maji.

Akasema: **Yeye ni duni mbele ya Allah kuliko hali hiyo**)), imepokewa na Muslim.

Al-Qaadhwi ‘Iyaadh Allah amrehemu amesema: "(Yeye ni duni mbele ya Allah kuliko hali hiyo), yaani: kuliko hali ya kufanya aliyoyaumba katika mikono yake [Dajali] ni yenye kupoteza waumini na yenye kutia shaka nyoyo za wenye yakini; bali itakuwa sababu ya wenye imani kuzidi imani, na wenye maradhi moyoni na makafiri kuzidi shaka, kama alivyosema yule ambaye [Dajali] alimuua kisha akamhuisha alipomwambia: (Katu sikuwa na elimu zaidi kukuhusu zaidi ya sasa)".

Wala kauli yake: (Yeye ni duni mbele ya Allah kuliko hali

1 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (19/205).

hiyo), haimaanishi: kuwa yeye hana chochote katika hayo; bali [lililokanushwa] ni kujaalia hiyo kuwa alama ya ukweli wake. Vipi iwe hivyo! wakati imejaaliwa alama ya uongo wake na ukafiri wake ni yenye kudhihiri katika maandishi atakayoyasoma hata asiyejua kusoma?! Ziada ya ushahidi wa uongo wake miongoni mwa kuumbwa kwake na upungufu"[1].

❉❉❉

1 Ikmaalul mu'lim bifawaaidi muslim (8/492).

## HUKUMU YA KUMFUATA MASIHI DAJALI

Fitina ya Masihi dajali ni kubwa, wala haijuzu kwa yeyote kumfuata kwa kiwiliwili chake wala kwa ulimi wake, hata akiwa anajua uongo wake kwa moyo wake.

Wala haijuzu kumfuata kwa sababu ya hali nzito na mahitaji makubwa, na kudhania kuwa kuna ruhusa ya kumsadikisha kama ilivyojuzu katika mengine.

Al-Mudh-hiry Allah amrehemu amesema: "Kauli yake: (Hakuna baina ya kuumbwa kwa Adam hadi kusimama Kiyama jambo kubwa zaidi kuliko Dajali), yaani: kwa ukubwa wa fitina yake, na uovu wa balaa yake.

Wala balaa yake, fitina yake na hofu ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie juu ya umma wake kutokana naye si kwa upande wa shubuha itakayokuta waumini wenye yakini na ujuzi wa Mola wao aliyetukuka na Sifa zake.

Kwani waumini hakika wameshamjua Allah aliyetukuka ujuzi ambao hauingiwi na dhana, wala haziwakabili shubuha; sababu Yeye aliyetukuka hafanani na kitu, wala chochote hakifanani Naye, na kuwa hakuna chochote kama mfano wake...

Na hakika si mengine ameonya umma wake kwa sababu kutoka kwake [Dajali] kutakuwa katika zama za shida na hali nzito, na kuwa watu watasibiwa na magumu, na kuwa yeye [Dajali] atamiliki mali na mifugo; basi inawezekana kaumu za watu wakamfuata kwa miili yao na ndimi zao, hata wakiwa wanajua uongo wake kwa nyoyo zao, na hakika Yeye aliyetukuka hana mfano wake chochote.

Na iwe kumsadikisha kwao na kumfuata kwao ni kwa uongo na kujificha, kwa taawili ya kauli yake aliyetukuka:

﴿إِلَّا مَنۡ أُكۡرِهَ وَقَلۡبُهُۥ مُطۡمَئِنُّۢ بِٱلۡإِيمَٰنِ﴾

{ila aliyetizwa nguvu na hali ya kuwa moyo wake ni mtulivu kwa imani} [An-Nahl: 106].

Na wanadhania yakuwa kuna ruhusa ya kumsadikisha, kama ilivyojuzu kwa wasiokuwa yeye.

Basi atakayemfuata Allah ataugeuza moyo wake, wala hatakubali kutoka kwake imani ya moyo wake kumwamini Allah, wala hatamkubalia udhuru katika nafsi yake, kwa sababu haikuja katika habari [Hadithi] ruhusa katika kumfuata kwa uongo.

Basi ndio Nabii akaonya kaumu yake, na akawahofia fitina yake kwa ajili ya hilo...

Basi vivyo hivyo yule aliyemfuata Dajali; kwa uongo na kutaka aliyonayo na kumuogopa, Allah ataugeuza moyo wake mbali na kuamwamini yeye, na wakufuru.

Na inawezekana iwe hali ya Dajali na kumfuata yeye ni miongoni mwa makatazo ambayo Allah ameshadidia ndani yake, wala hakujaalia ndani yake ruhusa, na kuwa atakayemfuata basi hatanufaika na imani yake, kama ilivyojaaliwa katika jambo la kutoka kwa jua upande wa magharibi fitina ambayo haikubaliwi baada yake imani ya ambaye hakuwa ameamini kabla ya hapo, hata likiwa hilo [la kuamini] ni katika hali ya kuwa na nguvu, siha na uwezekano wa kufanya"[1].

❊❊❊

1 Al-Mafaatiihu fii sharhil maswaabiih (5/409-410).

## WATU WAKALI ZAIDI DHIDI YA MASIHI DAJALI

Pindi atakapotoka Masihi dajali basi watu watakaokuwa wakali zaidi dhidi yake ni kabila la Banu Tamiim, Abu Huraira Allah amridhie amesema: ((Sijaacha kuwapenda kabila la Banu Tamiim kutoka nisikie matatu kutoka kwa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akiwa asema kuwahusu.

Nimemsikia akisema: **Wao ni watu wakali zaidi dhidi ya Dajali.**

Akasema: Na zilikuja sadaka zao, basi Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akasema: **Hizi ni sadaka za kaumu yetu.**

Na alikuwa mateka wao wa kike yuko kwa Aisha, basi Mtume akasema: **Muache huru, kwani huyo ni katika wana wa Ismail**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

Ibnu Hubairah (amekufa: 560 hijria) Allah amrehemu amesema: "Hili linajulisha ushujaa wao - yaani: kabila la Tamiim -, na kukita kwa imani yao mwisho wa zama pindi imani za watu zitatingisika"[2].

❉❉❉

1 Bukhari, nambari (2543), na Muslim, nambari (2525).

2 Al-Ifswaah 'an ma'ani sswihaah (7/6).

## SABABU ZA KUSALIMIKA KUTOKANA NA FITINA YA MASIHI DAJALI

Fitina ya Masihi dajali ni kubwa; na kinga kutokana nayo inakuwa baada ya tawfiki ya Allah kwa yanayofuata:

1- Kushikamana na Uisilamu, na kujihami na silaha ya imani, na kuwa na ilimu ya Majina ya Allah na Sifa zake nzuri zaidi; kwani Dajali ni mbovu wa jicho, na Mola Mlezi aliyetukuka si mbovu wa jicho.

2-Kujilinda na Allah kutokana na fitina yake.

Amepokewa Aisha Allah amridhie: ((Kuwa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiomba na hizi dua: **Ewe Allah mimi najilinda nawe kutokana na fitina ya moto, na adhabu ya moto.**

**Na fitina ya kaburi na adhabu ya kaburi.**

**Na kutokana na shari ya fitina ya ukwasi, na kutokana na shari ya fitina ya ufukara.**

**Na najilinda nawe kutokana na shari ya fitina ya Masihi dajali**)), wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea[1].

3- Kuhifadhi aya kumi za mwanzo wa Suratul Kahfi, au za mwisho wake.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atakayehifadhi aya kumi za mwanzo wa suratul Kahfi - na katika riwaya: za mwisho wa Kahfi -; atalindwa kutokana na Dajali**)), imepokewa na Muslim[2].

1 Bukhari, nambari (6377), na Muslim, nambari (589).

2 Muslim, nambari (809), miongoni mwa hadithi za Adu Dardaa Allah amridhie.

4- Atakayemsikia Masihi dajali basi amuepuke wala asimuijie; kwani mtu atamuijia - naye anajidhania kuwa ni muumini - na amfuate kwa shubuha anazozieneza.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Atakayemsikia Dajali; basi amuepuke, naapa kwa Allah, mtu atamuijia naye akijidhania kuwa ni muumini na amfuate, kwa shubuha anazozieneza**)), inepokewa na Abu Daauud[1].

Al-Mudh-hiry Allah amrehemu amesema: "Basi Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akithibitisha kuwa baadhi ya umma wake watamfuata Dajali tena kwa kuapa na Allah aliyetakasika, basi inampasa atakayesikia kutoka kwake asijimakini na fitina yake, na amuepuke umbali wa mashariki mbili, ndio asiingie katika fitina hiyo, kwani ni kubwa; bali ndio fitina kubwa zaidi, na itawaangamiza itakayowaangamiza, na mwenye kulindwa ni yule aliyelindwa na Allah aliyetakasika na kutukuka"[2].

5- Atakayekutana naye basi amsomee aya za mwanzo wa suratul Kahfi.

An-Nawwaas ibnu Sam'aan Allah amridhie amesema: ((Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alimtaja Dajali siku asubuhi moja, basi akateremsha sauti na kunyanyua hadi tukadhani yupo katika upande wa mitende.

Na pindi tulipomwendea alijua hilo ndani yetu, akasema: **Mna nini?**

---

1 Abu Daaud, nambari (4319), miongoni mwa hadithi za imran ibnu Huswein Allah awaridhie.

2 Al-Mafaatiih fii sharhil maswaabiih (5/435).

Tukasema: Ewe Mtume wa Allah, umemtaja Dajali asubuhi, ukateremsha sauti na kunyanyua hadi tukadhania yupo katika upande wa mitende!

Akasema: **Mimi nawahofia zaidi asiyekuwa Dajali, lau atatoka nami niko baina yenu basi mimi nitamghilibu kihoja nikiwa mbele yenu.**

**Na endapo atatoka nami sipo nanyi, basi kila mtu atajitetea nafsi yake, na Allah ndiye halifa**[1] **wangu juu ya kila Mwislamu**.

**Yeye ni barobaro mwenye nywele ngumu sana, jicho lake limechoza nje, kana kwamba mimi namfananisha na Abdul-uzzaa ibnu Qatwan.**

**Basi atakayekutana naye miongoni mwenu; amsomee aya za mwanzo wa Suratul Kahfi**)), imepokewa na Muslim[2].

Ibnul Jawzy (amekufa: 597 hijria) Allah amrehemu amesema: "Ama kuhusu hilo la aya kumi za mwanzo wa Kahfi; basi linalodhihiri kwetu katika hekima ya hilo: ni kuwa kauli yake aliyetukuka:

﴿لِّيُنذِرَ بَأۡسٗا شَدِيدٗا مِّن لَّدُنۡهُ﴾

{ili kitoe onyo ya adhabu kali kutoka kwake} [Al-Kahf: 2], ina dunisha adhabu ya Dajali.

Na kauli yake:

﴿وَيُبَشِّرَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ٱلَّذِينَ يَعۡمَلُونَ ٱلصَّٰلِحَٰتِ أَنَّ لَهُمۡ أَجۡرًا حَسَنٗا ۝ مَّٰكِثِينَ فِيهِ أَبَدٗا﴾

1 **Halifa wangu juu ya kila Mwislamu**: Allah ndiye mwenye kumnusuru kila Mwislamu na mwenye kumhifadhi.

2 Muslim, nambari (2937).

{na kiwabashirie Waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri * Wakae humo milele) [Al-Kahf: 2-3], inasahilisha subira juu ya fitina ya Dajali kwa yanaodhihiri miongoni mwa neema na adhabu yake"[1].

An-Nawawy (amekufa: 676 hijria) Allah amrehemu amesema: "Imesemekana sababu ya hilo ni yale yalio katika mwanzo wake [Suratul Kahfi] miongojni mwa maajabu na alama, basi atakayezinzingatia hatafitinika na Dajali, na vivyo hivyo mwishoni mwake"[2].

❉❉❉

1 Kashful Mushkil (2/165)

2 Sharhun Nawawy 'alaa Muslim (6/93).

## KUULIWA KWA MASIHI DAJALI

Baada kupatikana fitina kubwa [ya Dajali] katika ardhi, atashuka Isa ibnu Maryam salamu zimshukie sehemu za Damascus katika mnara mweupe, na amuuwe Dajali, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Basi katika hali ya kuwa wanajiandaa kwa vita**[1]**, wanapanga safu, swala itasimamishwa, na Isa ibnu Maryam swala na salamu zimshukie atashuka, na awaongoze katika swala, basi adui ya Allah [Dajali] atakapowaona, atayayuka kama inavoyayuka chumvi ndani ya maji, lau atamuacha atayayuka hadi aangamie, lakini Allah atamuuwa kwa mkono wa [Isa ibnu Maryam], na awaonyeshe damu yake katika kisu chake**), imepokewa na Muslim[(2)].

Na kumuuwa kwa mkono wa Isa ibnu Maryam; ni kwa ajili ya imani ya waumini izidi kuwa yeye alikuwa Dajali.

Na kuuliwa kwake kutakuwa Palestina, katika mlango wa Ludd - kaskazini magharibi ya Baytul Maqdis, iko mbali nayo kwa (50) km -, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema: ((**Ibnu Maryam atamuuwa Dajali katika mlango wa Ludd**), imepokewa na Tirmidhi[(3)].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Kushuka kwa Isa (Masihi wa uongofu) swala na salamu zimshukie katika masiku ya Masihi dajali (Masihi wa upotevu) kutakuwa katika mnara wa mashariki mjini Damascus, basi waumini wakusanyike kwake, na waja wa Allah wachamngu wamzunguke, atembee nao

1 Waislamu wanajiandaa kupigana na waroma.

2 Muslim, nambari (2897), miongoni mwa hadithi za Abu Hureira Allah amridhie.

3 Tirmidhy, nambari (2244), miongoni mwa hadithi za Mujammi' ibnu Jaariya Al-Answaary Allah amridhie.

akiwaongoza wakielekea upande wa Dajali, naye akiwa ameelekea Baytul Maqdis.

Basi amkute katika kijiji cha Afiiq[1] , na Dajali ashindwe [akimbie], na [Isa salamu zimshukie] ampate katika mlango wa mji wa Ludd, amuuwe kwa kisu chake akiwa anaingia [mji huo], na amwambie: Hakika mimi ninao dharuba moto kwako sitaikosa.

Na pindi Dajali atamkabili [Isa salamu zimshukie] atayayuka kama inavoyayuka chumvi ndani ya maji, basi amkute katika mlango [wa mji] wa Ludd, na hapo kiwe kifo chake"[2].

❉❉❉

1 **Kijiji cha Afiiq**: Mashariki ya ziwa la Twabariyyah, kiko mbali nalo kwa (5) km.

2 Al-Bidaayatu wan Nihaayah (10/206).


Nablus
Jaffa
Mlango wa Ludd
[Lod]
Ramallah
Baytil Maqdis
Bahari Maiti
Al=Khaliil
Gaza

## RAMANI ZA KUONYESHA SEHEMU ZILIZOTAJWA KATIKA HADITHI ZA MASIHI DAJALI

Mnao katika kiunganishi kinachofuata bayana na sherehe ya kueleza sehemu zilizotajwa katika hadithi za Masihi dajali kwa ramani za kisasa:

a-alqasim.com/addajjaal/

Tunamuomba Allah atulinde kutokana na fitina ya Masihi dajali, na atukinge na fitina za kudhihiri na za kufichika, na atufishe tukiwa Waislamu.

Na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad na watu wa nyumba yake na masahaba wake wote.

# FAHARISI YA MAUDHUI

UTANGULIZI ........................................................................................ 5
HATUA ZA KITABU ............................................................................... 7
JINA LA MASIHI DAJALI ...................................................................... 9
SABABU YA KUITWA «MASIHI DAJALI» ........................................... 11
KUTHIBITI HADITHI ZA MASIHI DAJALI .......................................... 12
MASIHI DAJALI NI KATIKA ALAMA KUBWA ZA KIYAMA ........... 15
KUTAHADHARISHA KUTOKANA NA MASIHI DAJALI ................... 17
HOFU YA MASAHABA ALLAH AWARIDHIE KUTOKA NA FITINA YA MASIHI DAJALI......................................................................... 21
SIFA ZA MASIHI DAJALI .................................................................... 23
HAKIKA YA MASIHI DAJALI.............................................................. 31
UDHAIFU WA DAJALI.......................................................................... 32
HALI YA MASIHI DAJALI HIVI SASA ................................................ 34
ALAMA ZA KUTOKA KWA DAJALI ................................................... 36
LINI ATATOKA MASIHI DAJALI? ....................................................... 48
SABABU YA KUTOKA MASIHI DAJALI............................................. 51
SEHEMU ATAKAYOTEKEA MASIHI DAJALI .................................... 52
HALI YA WATU PINDI ATAKAPOTOKA MASIHI DAJALI. .............. 61
MWENDO WA KASI WA MASIHI DAJALI KATIKA ARDHI. ............ 67
MASIHI DAJALI HATOINGIA MAKKAH NA MADINAH. .................. 69
MADINAH HAINGII NDANI YAKE HOFU YA MASIHI DAJALI....... 70
SEHEMU ATAKAYOSHUKIA MASIHI DAJALI KANDO YA MADINA ............................................................................................................ 72
MDA WA KUKAA MASIHI DAJALI KATIKA ARDHI ......................... 77

FITINA YA MASIHI DAJALI.................................................................. 78

HEKIMA KATIKA FITINA YA MASIHI DAJALI .................................. 83

HUKUMU YA KUMFUATA MASIHI DAJALI ....................................... 85

WATU WAKALI ZAIDI DHIDI YA MASIHI DAJALI ............................ 87

SABABU ZA KUSALIMIKA KUTOKANA NA FITINA YA MASIHI DAJALI. ........................................................................... 88

KUULIWA KWA MASIHI DAJALI.......................................................... 92

RAMAZIBZA KUONYESHA SEHEMU ZILIZOTAJWA KATIKA HADITHI ZA MASIHI DAJALI .................................................................. 95


FIHRISI YA MAUDHUI......................................................................... 96

Taasisi ya 'twaalibul ilm' ya kunushuru na kugawa.


00966506090448

# أحاديث الدجال في السنة النبوية

## مترجم بالسواحلية





**NI KATIKA MATOLEO YETU**











a-alqasim.com
FawaidAlQasim